

MASWALI NA MAJIBU JUU YA WAEBRANIA, SEHEMU YA II

✎ Nataka kwanza kumshukuru kila mmoja wenu aliyepata ujumbe wa “mwombeeni mke wangu.” Yeye alikuwa mahututi sana sana. Hatukujua ilikuwa nini, na hatujui nini ilitendeka, ni kutapika sana hata karibu apotewe na fahamu, na joto yapata kipimo cha mia na tano, ilibidi afunikwe na mablanketi ya barafu. Kwa hivyo . . . bali amepona sasa. Joto lote limekwisha, naye amepata nafuu. Kwa hivyo yeye ni mdhaifu sana, amepoteza karibu ratili kumi, nadhani. Haja . . . Usiku huu amemeza mlo wake wa kwanza tangu Jumapili. Na kwa hivyo alikuwa mgojwa sana, nasi tulimtumainia Bwana kwa ajili yake, naye akampa nafuu. Sasa tunataka kuwaambia muendeleo kuomba kusudi nguvu zake zimrudie.

³⁰⁴ Na sasa, mwishoni mwa juma hili lijalo, Bwana akipenda, yanibidi kwena Miami. Rafiki yangu mzee, Ndugu Bosworth, anaenda Nyumbani, naye ana umri wa miaka mia sasa. Basi aliniita, akisema, “Ndugu Branham, njoo unione mara moja, nataka kukwambia jambo fulani kabla sijaondoka.” Naye . . . Vema, nafikiri anataka kuniombea, na kuniwekelea mikoni kabla hajaondoka, mwajua.

³⁰⁵ Nami na—natumaini naweza kumaliza siku zangu nikiwa mwenye sifa mjema kama F.F. Bosworth. Katika watu wote niwajua duniani, kila mtu niliyepata kukutana naye duniani, sijawahi kukutana na mtu niliyopendelea kuwa kama yeye, kama F. F. Bosworth; kama—kama mhudumu, namaanisha. Sijawahi kusikia mtu mmoja, ulimwenguni kote, mahali po pote, aliyewahi kumtaja F. F. Bosworth ila kwa kila hali kuwa “Mkristo,” na kila hali “ndugu halisi.”

³⁰⁶ Kutengana huacha nyuma nyayo kwenye zile changarawe za nyakati. Yeye ni ndugu wa ajabu, yeye ni mzee sana sasa, karibu miaka mia. Kwa hivyo yuaenda Nyumbani, hivyo tu, naye aliniambia. Alijua yuaenda, naye alikuwa tu akingoja. Alisema wakati mzuri sana wa maisha yake ni hivi sasa anapongojea tu, bali alisema anajua yuaondoka.

³⁰⁷ Nilisema, “Sina budi kwenda Michigan juma hili, Ndugu Bosworth.”

³⁰⁸ Naye akasema, “Vema, usikawie sana, Ndugu Branham, sitadumu zaidi. Nadhoofika wakati wote.”

³⁰⁹ Kwa hivyo yeye amekuwa rafiki msiri wangu sana, kutokwenda kule. Basi, ikinibidi kuruka kwa ndege, nita—nitarudi kwa ndege na labda nirudi Jumapili usiku kwa vyo

vyote vile; la sivyo, vema, itanibidi nisafiri kwa motokaa, na huenda ikanichukua muda mrefu zaidi kidogo.

³¹⁰ Basi mwombeeni Ndugu Bosworth. Ombeni tu kwamba Mungu... naye atakapomchukua huyu mzee shujaa, kuwa atamtumia gari la moto likampandishe, ona. Nampenda, amekuwa kama baba kwangu mimi.

³¹¹ Mzee mwingine... yeye na Ndugu Seward. Ni—ninawapenda wazee, na—nawapenda. Basi mzee Ndugu Seward, yeye alilala vivyo hivyo, pia. Ingawaje, Ndugu Seward hakuwa mzee hivyo, sidhani, kama Ndugu Bosworth.

³¹² Basi mwombeeni Ndugu Bosworth. Kila kitu si waridi kote mahali pale, lakini ni—ni... Yeye anahitaji maombi yenu, bali si kwa lingine ila tu... kwamba Mungu atamruhusu aondoke kwa amani.

³¹³ Basi... Kisha tunataka kukumbuka, pia, kuwa kesho, Bwana akipenda, tutamzika mmoja wa rafiki zetu wa kanisa hili, Ndugu Sol Coates. Yeye amekuwa hapa mara kadha, alifanya kazi posta kwa miaka mingi. Naye alifariki kwenye hospitali ya Veteran usiku uliopita. Mimi na Ndugu Cox tuliondoka tukaenda kumwona, naye alikuwa... hawezi kabisa. Naye amekwisha ondoka sasa, Mkristo. Nasi tutamzika kwenye makaburi ya Coot kesho alasiri saa saba, mimi na Ndugu Neville. Kwaya ya Neville ya watu watatu itaimba; nasi tutashirikiana kwa ibada, mimi na Ndugu Neville. Yaani, sikujua tulifanya mipango vipi, na kwa ajili ya Meda. Na kwa hivyo, basi, mazishi yake yatakuwa kesho jioni saa saba alasiri, kwenye makaburi ya Coots.

³¹⁴ Ndiposa, saa nane, Ijumaa, Bw. Wheller. Tulimwita Pod Wheller; yeye ni, nasahau jina lake hasa... Basi, mwajua, ni—niliona hayo kwenye gazeti nami sikujua ilikuwa nani, hata nilipotambua. Yeye alikuwa jirani yetu kwa miaka kadha, na—naye ameaga dunia. Alikuwa papa hapa mbele ya kanisa, usiku mwingine, nami nilikuwa nikijaribu kumleta kanisani. Usiku mwingine, yapata majuma matatu yaliyopita, alisimama papa hapa, nami nilikuwa nikijaribu kumshawishi aje kanisani. Kwa sababu, sidhani alienda kanisani au alikuwa na maungano ya aina yo yote, lakini ana kijana aliye mhubiri Mbatisti. Lakini yeye hakuwa na maaungano yo yote, kadiri nijuavyo mimi, naye amekwenda kukutana na Mungu. Kwa hivyo hayo yatakuwa Ijumaa alasiri saa nane kwenye makaburi ya Coots. Kisha, Ndugu Neville na wengineo watakuwa wakiimba, huko kwenye mazishi hayo.

³¹⁵ Kwa hivyo basi, kama ye yote wenu akitaka kuhudhuria ibada hizo, ni kesho saa nane... au kesho saa saba. Nafikiri ndivyo ilivyo. Sivyo, Ndugu? Halafu, saa nane, hayo mengine. Sivyo? Saa nane kwenye makaburi ya Coots.

³¹⁶ Basi sasa, Jumapili asubuhi... Jumamosi ni mahubiri ya redioni. Na Ndugu Neville labda atawajulisheni, ifikapo wakati

huo, mambo yalivyo. . . iwapo tutakuwa na ibada ya uponyaji Jumapili, au tutarudi wakati gani tukisafiri kwa ndege hadi—hadi Florida kumwona Ndugu Bosworth. Sijui nitakavyoagana naye, yeye ni mzee rafiki msiri wangu sana. Na labda ndio wakati wa mwisho kukutana, Bwana akipenda, humu duniani. Naye. . . Sijui kama naweza kuachana naye, lakini, mwajua ilivyo, una mambo mengine yakupasayo kufanya.

³¹⁷ Sasa kuna neno moja ningetaka kusema hali kukiwa hamna watu wengi sana, na watu walio rafiki zangu.

³¹⁸ Nina furaha kumwona Dada Smith hapa. Ni mara ya kwanza kumwona baada ya muda mrefu. U hali gani Dada Smith? Mwaka mzima, jamani, naamini ndio wakati wa mwisho niliokuona. . . [Dada Smith anena—Mh.] Kule Benton Harbor, natumaini kwenda kule wakati mwingine. Naam. Naamini wakati wa mwisho niliokuona, ilikuwa kwenye mazishi kule Louisville. Nami namkumbuka Dada Smith vema sana. Jinsi tuli. . . nilikuwa nikija na kumbeba kwa gari tulipokwenda kanisani. Lami ya kale ya makaa ya mawe ikining'inia kule nyuma na vikingio vikirushwa juu chini, na baridi; nami, mguu mmoja nje. Jamani, maji mengi yametiririka kule mtoni tangu wakati huo, Dada Smith. Naam, bwana. Vema, twamshukuru Bwana kwa ajili ya kumbukumbu hizo za thamani, na tungali tunampenda.

³¹⁹ Jambo moja, mtu fulani huenda akashangaa, usiku uliopita. . . nilikuwa nikiongea na Ndugu Fleeman hapa kwenye barabara ya mji. Na wakati mwingine mtu fulani alisema, “Mara tu baada ya ibada, nini humfanya Ndugu Branham aondoke mara moja?”

³²⁰ Sababu yake ni kwamba, mke wangu yuko peke yake. Ona? Basi nikianza kuongea, nitaongea nusu usiku, naye ndiye huyo pale, ameketi hapo peke yake karibu wakati huo wote. Basi hiyo ndiyo sababu mimi huondoka upesi, kurudi alipo, mwaona, wakati wa usiku; kwa sababu nikianza kuongea, naongea kwa muda mrefu zaidi. Nitaongea na *huyu* kwa nusu saa. Siwezi kupita tu na kusema, “Habari *yako* usiku huu? *U* hali gani. Hujambo *wewe*?” Sifanyi hivyo. Nasimama na kuendelea kuongea; na mtu fulani anaanza kuongea jambo fulani, ndiposa niko hapo kwa saa moja. Ona? Basi hiyo ndiyo sababu yake, yeye huketi akingoja na kadhalika. Naam, hivyo ndivyo ilivyo. Sikutaka mfikirie ni kwa sababu sikutaka kukutana na rafiki zangu na kuamkuana nao, na kuonyesha ushirika wetu na kadhalika, bali hiyo ndiyo sababu yake.

³²¹ Kwa hivyo, sasa, kila mtu awaombee wagojwa na wanaoteseka.

³²² Pia mke wa Harvey yuko katika shida hiyo yote, anapata nafuu. Naam, Bwana. Nami sioni. . . ni. . . Basi huenda pakaweko, kwa kadiri nijuavyo, mtu fulani, daktari hapa. Basi

iwapo nimekosea juu ya hii jukwaa, Mungu anisamehe. Bali naamini Mungu atawahukumu madaktari hao kwa ajili ya yale waliyomtendea mwanamke huyo. Na—naamini katika upasuaji, naamini katika madawa. Bila shaka naamini. Nafikiri Mungu aliwatuma hapa kutusaidia, kama vile tu alivyowatuma mafundi wa motokaa na na kadhalika. Lakini maskini mwanamke huyo, daktari alimkatia tamaa, kasema, “Amejawa na kansa, haiwezekani.” Maskini mama mwenye watoto wengi.

³²³ Nikamwendea, na kujaribu kumweleza jinsi ambavyo kwa maombi... Na—naye ni mwanamke kijana, yapata miaka ishirini na mitano. Na jinsi Mungu alimponya mtoto wake mchanga, anaitwa “mtoto wa kimiujiza” kwenye hospitali ya watoto sasa, ugojwa wa ngozi inayofunika ubongo. Naye alikuwa mahututi sana huyo mtoto mchanga, kisha Baba akamponya papo hapo. Hao, madaktari, hawakuweza kuelewa. Nikamwendea Bi Harvey, nami nilisema, “Sasa, Bi Harvey, je, madaktari walikukatia tamaa?”

³²⁴ “Naam, Bwana, Ni...”

³²⁵ Basi mumewe akasema, “Naam, hakuna la kufanya, yeye amelemewa kabisa na kansa.”

³²⁶ Nikasema “Vema, sasa kile tunachotaka kufanya, ni kumwamini Mungu, ya kwamba Mungu ata—ataponya... atakuponya.” Nami nikasema, “Huwa ya kwamba, huenda hiyo kansa isiondoke mara moja: bali tukiomba, basi uhai wa hiyo kansa unaondoka. Huenda ukawa mgojwa bado kwa muda fulani, na—na” nikasema, “huenda maumivu yakaondoka papo hapo.” Nami nilisema, “Kisha baada ya siku chache huenda ukawa mgojwa zaidi ya ulivyopata kuwa.” Lakini nikasema, “Yakubidi uikabili hiyo kansa kwa imani yako.” Nikasema, “Kansa ikiishi, wewe utakufa. Kansa ikifa, utaishi.” Basi nikasema, “Sasa tutaomba.”

³²⁷ Nasi tuliomba, na kila dalili niliyoona, Mungu aliugusa mwili wa mwanamke huyo. Na mara akajisikia hajambo, akaenda kumwona mama yangu, akawazuru majirani, (alipokuwa bado yu mnyonge hivyo) hakuwa na maumivu yo yote. Ndiposa baada ya siku tatu hivi akaanza kuwa mgojwa tena.

³²⁸ Hatimaye halmashauri ya mji ikasema wangelilipia “gharama za daktari, iwapo madaktari wangeipasua.”

³²⁹ Basi kama nimekosea sasa, Mungu anisamehe. Lakini walimchukua huyo mama kijana, wakamfanya kama “Mwili wa kufanyia majaribio.” Wakampeleka kule na hata wakayaondoa matumbo yake tumboni mwake, na kila kitu. Wakaviondoa vibofu na matumbo, na kuviweka upande. Naye alikuwa kwenye meza ya upasuaji kwa masaa tisa na kitu. Muuguzi fulani alisema, “ilionekana kama machinjioni, jinsi walirusha-rusha matumbo yake huku na huko, na kuweka vifuko vya uzazi

vya plastiki na mirija ya plastiki.” Hilo ni wazi, bali ni kweli. Na matumbo ya plastiki na vitu kama hivyo, na kumwacha huyo mama amelala hajiwezi, maskini mama. Nasema, nionavyo mimi, hao madaktari wana hatia ya mauaji.

³³⁰ Yeye alimwambia, akasema, “Ndugu Branham aliniombea.” Kisha kasema, “Tutaamini kuwa kansa yetu . . . kuwa hiyo kansa imekufa.”

³³¹ Kasema, “Nina habari kwako, ‘Kansa yako ni hai.’”

³³² Yeye angejua? Ilikuwa mle ndani, hamna picha ya X-ray inayoweza kuiona. Kansa ni . . . Huwezi kuitambua kansa kwa kutumia X-ray, yenyewe ni mwili, huwezi kuiona. Jambo pekee walilofanya, walimpasua huyo mwanamke na kumkata-kata vipande. Hivyo tu. Basi kama ningelikuwa maskini mama yule, ningemwacha tu ajaribu imani yake kwa Mungu badala ya kumfanya kama “mwili wa kufanyia majaribio” mtu kama huyo. Naam, kama ni—kama nimekosea, kama ni—kama nina nia bovu, nataka Mungu anisamehe, mwaona. Kwa kuwa sitaki ninyi mfikirie kwamba siamini katika upasuaji au kuamini madaktari na kadhalika. Naam. Lakini nafikiri yakubidi ujue unachofanya kabla hujamwingilia mtu, si kuwatumia tu kwa kufanyia majaribio hivyo. Naam. Basi sasa, bila shaka, yeye hawezi kuishi. Hivyo tu. Akiishi, hakika utakuwa mmoja wa miujiza mikuu zaidi iliyowahi kutendeka. Mwanamke yule alipotazama na kuona matumbo yake yakiwa upande mmoja, na figo zake zikirukaruka upande mwingine, alizirai tu *hivi*, akazirai . . . Naam, halikuwa jambo . . . maskini huyu akazimia. Na karibu tu mama wa umri wa miaka ishirini na miwili au ishirini na mitano, mwenye watoto watatu wanne wa kulea. Jambo la kusikitisha sana ambalo nimewahi kusikia maishani mwangu. Nilisema, “Nionavyo mimi, huyo daktari ana hatia ya . . .” Kama alimchukua mwanamke yule tu kufanyie majaribio kwa sababu mji ungeyagharimia, basi hilo ni kosa, haipaswi kukubaliwa.

³³³ [Mtu fulani anauliza iwapo Mungu anaweza kumrudisha tena mwanamke yule—Mh.] Vema, nakwambia, Ndugu, li . . . si lisilowezekana. Na ni—na . . . ina—inawezekana, na pia yamkini. Kwa sababu namjua mtu aliyekakwa mkono, kule California (ninyi nyote mnaifuata gazetini), akaombewa, na mkono *huu* ulikatiwa juu *hapa*, na umekua hata vidole tayari vinaota sasa; kupitia kwa kivi, kupitia kwa kiwiko hata kwa kiganjo, na sehemu za konzi zilikuwa zimeotesha vidole tena, mwaona. Yako katika, naamini, *Mbiu ya Imani* kila mwezi. Hata anapoutoa mkono wake *hivi*; mahali mkono wake upokatiwa panaonekana, ambapo uliotea. Kila mwezi jinsi unavyoota, kwa muda wa mwaka mzima.

³³⁴ [Mtu yule anena mkutanoni tena—Mh.] Bila shaka. Naam. Naamini . . . Ni—ni—ni jambo adimu, ona, ni jambo adimu sana. Si mara nyingi nimesikia hayo. Naam, Ndugu Bosworth

alimwombea mwanamke fulani usiku mmoja. Nami nilikuwa na mmoja katika mkutano wangu. Bali wa Ndugu Bosworth ulikuwa papo hapo; wangu ulichukua muda mrefu kutendeka.

³³⁵ Yeye alimwombea mwanamke mmoja. . . Naam, niliusoma ushuhuda wa huyo mwanamke. Alikuwa na kansa, bila mapua; ilikuwa imekwisha kula mapua yake. Na asubuhi iliyofuata mwanamke huyo alikuwa na mapua. Sasa, najua hili. . . Sasa, huyo ni Ndugu Bosworth, katika kitabu chake kiitwacho *Kristo Aliye Mponya*, naamini, au, *Mfariji*, mojawapo. Sasa, yako kwenye ushuhuda wa mwanamke yule, pamoja na jina na anwani yake. Naye ana majirani na madaktari na kadhalika kuthibitisha hilo, kuwa lilitendeka.

³³⁶ Sasa kule Little Rock, Arkansas, usiku mmoja chumbani, nilikuwa nikiombea huko. . . si Little Rock, bali ni Jonesboro. Ndiko nilikoombea. . . nilisema, “Nitakaa hata nitakapomwombea mtu wa mwisho.” Niliikuwa jukwaani siku nane mchana na usiku, ona. Ndiposa. . . kisha mwanamke mmoja akaja mle chumbani, amejifunga kitambaa *hivi*, nami nilidhani analia. Nikasema. . . Ed, nafikiri ilikuwa saa nane au saa tisa usiku, nikamwambia, “Usilie, dada, Mungu ndiye mponyaji.”

³³⁷ Akasema, “Silii, Ndugu Branham.” Akakiondoa; hakuwa na mapua, ona. Daktari alikuwa amesema. . . Kansa imekwisha kula ule mfupa wake mweupe. . . ulikuwa ukionekana. Nami nikamwombea, na kumsihi Bwana amponye.

³³⁸ Na yapata majuma manne au matano tangu wakati huo, nilikuwa Texarkana. Na alikuweko mwungwana aliyevalia nadhifu ameketi pale, akasema, “Naweza kusema neno, Ndugu Branham?”

³³⁹ Mara tu alipofika jukwaani, mmoja wa mabawabu akajaribu kumnyamazisha. Nikasema, “Vema, hebu tuone.”

³⁴⁰ Yeye akasema, “Wamtambua huyu bibi kijana?”

³⁴¹ Nikasema, “La, simtambui.”

³⁴² Huyo mwanamke akasema, “Ukiitazama picha hii utaitambua.” Naye alikuwa mnyongaji kule—kule Texarkana, na huyo alikuwa mama yake mwenye pua jipya lililoota, lilifanana kabisa na lile lingine.

³⁴³ Sasa hiyo yaonyeshe kuwa Mungu. . . nimeona ikitendeka. Naam Mungu angemfanyia hayo mpendwa Bi. Harvey. Nami naomba amfanyie kwa maana maskini mtu huyo yuataka kuishi.

³⁴⁴ Ndugu Tony, ulikuwa na jambo fulani? [Ndugu Tony atoa habari ya uponyaji fulani—Mh.] Naam. Amina. Amina. Naam, hilo ni zuri, pia. Naam, Yeye atafanya hivyo bila shaka, Yeye ni mponyaji.

³⁴⁵ [Mtu mwingine afafanua—Mh.] Naam. Naam. Ndivyo Ndugu. Amina. Bila shaka. Naam. Hakika ninge. . . Natumaini

Mungu atakurudishia, mwanangu, waweza kuichukua tena na kumwonyesha. Naam, hasa. Ni kwa ushuhuda wa utukufu wa Mungu, naomba Mungu atalitenda. Ee, Yeye—Yeye... Iwapo Yeye ni Mwenyezi Mungu, Yeye aweza kufanya mambo yote. Kama hawezi kufanya hivyo, mambo yote, basi Yeye si Mwenyezi Mungu.

³⁴⁶ Kuna kitu fulani kilichotufanya tulivyo, jinsi tulivyo, au tungalikuwa na—na kichwa kama cha ndege, au kitu kama hicho; kama kusingalikuwa na busara kuu nyuma yetu kumfanya kila mmoja wetu kwa umbo fulani, kuumba mti ulaya, mlobna, mtende, na—na kutofautisha kati yao jinsi—jinsi vilivyo. Kutotuumba kwa... wengine na sufu, na wengine na manyoya, na wengine na ngozi, ili ninyi... Ona, ni—ni busara kuu iliyotenda hayo—inayoongoza hayo. Bila shaka Yeye anashikilia vyote mkononi Mwake. Nami najua Yeye aweza kufanya mambo yote. Basi tutamwombea, tutaomba.

³⁴⁷ [Mtu mwingine anena mkutanoni—Mh.] Sawa. Tuna... .

³⁴⁸ [Dada Snyder asema, “Ndugu Billy, tafadhali—Mh.]. Naam, mama, vema, endelea. [Dada Snyder atangaza “amepona” Ndugu Branham alipomwombea Jumapili iliyopita—Mh.] Amina. Wajua, nimejaribu kuwaza, Dada Snyder, wakati mmoja nilipokuwa nimesimama hapa katika upako huo, nilidhani... Nilimwambia Ndugu Cox, nilisema, “Sitajaribu tena hiyo mikutano ya utambuzi kule Maskanini.” Ee, hamjui jinsi huyo Shetani huniumiza wakati mwingine kwa huo, dada. Jinsi—jinsi afanyavyo! Akiniambia kuhusu huu utambuzi.

³⁴⁹ Na hapa, nilitambua kuwa dada ya Bi. Wood hapa... Sikuwa nimewahi kuona ye yote wa watu wao. Wengi wao waliponywa wakati huo, na kila mmoja... Naam, mwajua ni sehemu kubwa sana ya watu hao iliyoponywa. Na baadaye... Jambo geni sasa; dada yake, nimekula chakula cha kutwa pamoja naye usiku mmoja, yapata majuma mawili hapo kabla... Ee, kule mbali milimani Kentucky, nami—nilijua yeye alikuwa na sauti kama ya Bi. Wood, na haikuwa nyepesi sana chumbani. Nami sikumjali sana kwa vyo vyote vile, niliongea zaidi na mumewe, mama huyo aliachwa. Tulienda nje tukaketi na tukala, tukaingia tena, nikaongea na mumewe, nikaamka na kuondoka nje. Na Mungu ambaye ni Hakim wangu halisi ajua (nikisimama karibu na mimbara hii) sikumtambua mwanamke huyo kamwe.

³⁵⁰ Ndiposa ibada ya uponyaji ilipokwisha, nikatoa wito wa madhabahuni wenye dhambi watubu. Naye aliupinga kwa kiburi sana; kisha akatubu na kuyatoa maisha yake kwa Kristo, akainua mkono kuwa angemtolea Kristo maisha yake, huku akilia. Baada ya upako huo wote kwisha; kutoa wito wangu wa madhabahuni, na kadhalika. Ndiposa, nikageuka, ono likaja, nami nikamwona ndugu yake; ilikuwa dada, huyu alikuwa dada yake, wote pamoja.

³⁵¹ Nami nilidhani ni mke wa Charlie, kwa sababu nilijua alipoketi pale mezani juzi, kule nyu—nyumbani mwa Charlie . . . Mke wake mpendwa, mwembamba, Bwana alinionesha shida aliyokuwa nayo. Na tangu wakati huo, Bwana akaugusa mwili wake, ameketi papo hapo mezani mwake sasa. Tony, tulipokuwa kule, kule chini, kuwinda kuchakulo. Kisha Bwana akaugusa mwili wake na kuondoa kitu hiki alichokibeba maishani mwake mwote . . . maishani mwake mwote, akakiiondoa, akiketi pale. Na mwanamke yule mpendwa kila mara alikuwa akila kwenye upande wa pili wa meza, lakini leo, yeye alikuja papo hapo, naye akasogesha kiti chake, na kulia karibu nami. Yeye hakujua kile alichokuwa akifanya. Mume wake ameketi *hivi*, na Ndugu Bank ameketi pale, nasi tukiongea. Naye akaja hapo, akatwaa kiti chake, na kukiweka hapo karibu nami. Basi hiyo ilikuwa na kusudi, Bwana akaonyesha ono papo hapo. Nami nikamwita mumewe nje, kwa kuwa ilikuwa ni shida ya kike, nikaanza kumwambia mumewe kile kilichotendeka. Yeye akasema, “Ndugu Branham, hivyo ndivyo ilivyotendeka hasa, vivyo hivyo hasa.” Kisha akamwambia mkewe, naye Bwana akamponya. Vema.

³⁵² Ndiposa baada ya ibada kwisha usiku wa juzi, na huyu dada mwingine, nilimwona huyu maskini Charles pamoja na mwanamke huyu. Nikawazia, “Hapana budi huyu ndiye mke wake; ila mke wake ana nywele nyeusi.” Kisha nikaona hilo ono likielekea pembeni hapa. Naye alikuwa ameketi pale huku akipangusa macho yake kisha Bwana akaonyesha ono alipokwisha kuwa . . . ule mwito wa madhabahuni . . . huo mkutano wa maombi ulipokwisha, kule kuponywa kwa wagojwa, na mwito wa madhabahuni umekwisha kufanywa, naye Mungu akangoja hata alipotubu na kutoa maisha yake Kwake ndiposa akageuka na kumponya. Naye alikuwa na . . . shida zake zilikuwa zimeongezeka kwa miaka mingi. Pia amedhoofika sana, na kadhalika, hata miguu yake ilikuwa imekunyanzika mahali ambapo ilikuwa imetolewa (ile sumu) mwilini mwake. Anajisikia vizuri zaidi ya vile alivyokuwa kwa miaka mingi, ona. Na jinsi Bwana kwa neema Yake ya ajabu hufanya hayo! Nadhani hiyo ndiyo hadithi ile; sivyo, Dada Wood? Na jinsi Yeye hutenda! Baada . . . Wasemaje? [Dada Wood asema, “Yeye alipoteza ratili saba juma lililopita”—Mh.] Ratili saba kwa juma. Ee, Yeye ni Mungu! Sivyo?

³⁵³ Sasa nitawambia, sababu nilimwambia Ndugu Neville . . . nilidhani labda yeye alikuwa na ujumbe kwa ajili ya usiku huu. Akasema, “La,” hakuwa nao. Nami nina maswali machache hapa yaliyobakia, nilijisikia yanibidi kufika humu na kujibu haya maswali. Basi ninayo mawili matatu zaidi ambayo labda sitayafikia usiku huu.

³⁵⁴ Nataka kuwaonyesheni mengine yaliyoletwa toka kwa muhubiri. Ndugu Neville ndiyo kwanza . . . au Beeler ameniletea

sasa hivi. [Ndugu Branham ayajibu maswali haya manane yafuatayo katika Sehemu ya III kuanzia aya ya 688, kama swali nambari 67 hata 74—Mh.]:

Je, yale mawe ya Ufunuo 21:19 na 20 yanaonyesha nini?

Eleza wale wenye uhai wanne wa Ufunuo 5... Yeye anamaanisha, 6; si Ufunuo 5, ni 6, nadhani.

Na hawa wazee ishirini na wanne ni akina nani?

Nini maana ya ile kamba nyekundu ya Mwanzo 38?

Zile zawadi zitatumwa wapi zinazohusu kifo cha wale wawili wa Ufunuo 11?

Watakatifu watakuwa wapi baada ya ule utawala wa miaka elfu moja? Watakuwa na mwili wa aina gani?

Tutahukumuje malaika?

Ni nywele gani zinazowapendeza malaika wa I Wakorintho?

³⁵⁵ Nena kuhusu yaliyo mazuri, hayo ni mazuri. Labda sitayafikia usiku huu, lakini Bwana akipenda, nitajaribu kuyajibu wakati tutakapokusanyika kwa ajili yake.

³⁵⁶ Ninayo mazuri sana ndani humu usiku huu, kwa hivyo tutaomba sasa na kumuuliza Bwana atusaidie, tupate kuyaingilia kwa muda wa, ee, dakika thelathini na tano, arobaini.

³⁵⁷ Sasa, Baba wa Mbinguni uliyehimidiwa, tuna shukrani Kwako kwa yote uliyotufania. Na, ee, ni ajabu sana jinsi neema yako hutushukia. Nawaza sasa, usiku uliopita, na huyo maskini mwenzi wangu, lo, mgojwa sana, nawe ukajitokeza. Joto lake likaanza kupungua tangu saa iyo hiyo, na limekwisha kabisa sasa. Nakushukuru. Na. . .naomba tu kwamba utakuwa na kila mmoja aliye mhitaji usiku huu. Nasi hatujui sana, hata shida inapoingia nyumbani mwetu, faida yake, ombi ndogo. Ee Mungu, kile. . .jinsi—jinsi ulivyo halisi. Katika saa hiyo ambayo daktari ataondoka, na kusema, “Sijui, sijapata kuona kitu cho chote kikitenda hivyo,” ndiposa Bwana Yesu anajitokeza jukwaani.

³⁵⁸ Ee Mungu, Wewe u halisi sana kwetu, hivyo basi twashukuru sana. Twaomba utusamehe uvivu wetu, na upumbavu wetu. Na, ee, hebu na utukumbuke sisi, Bwana, kwa maana sisi ni miili ya kibinadamu katika dunia hii yenye giza, ulimwengu wa giza na dhambi na ghasia. Nasi twatazama kupitia kwa pazia, kama wasemavyo, iliyotufunika uso, nasi twaona tu na kujua jinsi tujuavyo kibinadamu hapa. Bali hivi karibuni pazia hiyo itakapoondolewa, tutaona uso kwa uso na kujua kama tunavyojuliwa. Hiyo ndiyo siku tunayoitarajia.

³⁵⁹ Nasi twaomba Baba, sasa, kwamba utatusaidia tunapojaribu kuwapa watu Neno la Mungu, kulingana na haja zao. Tuondoshee magojwa yote. Tunakuhitaji, Bwana. Nasi

tunaomba ya kwamba utatujalia. Na tupewe neema Yako, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

³⁶⁰ Sasa katika kujibu maswali, mimi siye bora sana nchini, mwajua. Bali nitayajibu tu kadiri nijuavyo.

³⁶¹ Hapa kuna lile nililoanza usiku uliopita, na ikanibidi kukoma:

60. “Kwa maana katika Roho Mmoja sisi zote tulibatizwa kuwa mwili wa Kristo.” (Nyote mnakumbuka kuwa hilo ndilo swali nililokuwa nikijibu. Sasa, hilo lapatikana, bila shaka, katika I Wakorintho 12)... **Tunapo... tunapozaliwa mara ya pili, hili hutendeka. Huu... Je, huu ndio Ubatizo wa Roho Mtakatifu, au kunao ubatizo ujao baadaye, au huku ni kujazwa?**

³⁶² Naam, hili ni swali kweli kweli, nasi tungetumia wakati wetu uliobaki kwa swali lili hili, na usiku huu na kasho usiku na kadhalika. Lingegusa... lingekuwa—lingechukua na kufungamanisha Biblia nzima pamoja. Kila Andiko halina budi kulingana vilivyo na kila Andiko lingine katika Biblia.

³⁶³ Lakini kwa kujaribu tu kufupisha, dhahiri nijuavyo, la; unapomwamini Bwana Yesu Kristo, basi umezaliwa mara ya pili. Unapomwamini Bwana, unapokea wazo jipya, uzima mpya, bali hiyo si Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ona? Umezaliwa mara ya pili unapoamini, una Uzima wa Milele. Ni kipawa cha Mungu ambacho amekupa kwa neema kuu kwa kukubali kile kipawa anachokupa. Ona, “Yeye asikiaye Maneno yangu na kumwamini yeye aliyonipeleka, yuna Uzima wa Milele.” Yuna uzima wa milele; huko ndiko kuzaliwa mara ya pili, umeongoka, inamaanisha “umegeuzwa.”

³⁶⁴ Bali Ubatizo wa Roho Mtakatifu unakuvingiza katika mwili wa Kristo, tayari kupokea karama kwa ajili ya huduma. Haukufanyi kuwa Mkristo zaidi; unakuvingiza tu katika ule mwili wa karama. Ona? “Sasa, kwa Roho mmoja” (1 Wakorintho 12) “sisi sote tumebatizwa kuwa mwili mmoja. Sasa,” Paulo asema, “kuna karama mbalimbali, na katika mwili huu mna karama tisa za kiroho.” Na katika mwili huu... Yakubidi ubatizwe katika mwili huo kusudi upokee mojawapo wa karama hizi. Hizo huambatana na huo mwili.

³⁶⁵ Lakini, sasa, kuhusu kuwa na Uzima wa Milele na kuwa Mkristo, unakuwa Mkristo mara tu unapoamini. Sasa, huko si kujifanya mwamini, huko ni kumwamini Bwana Yesu kabisa na kumkubali Yeye kama Mwokozi wako binafsi; umezaliwa mara ya pili papo hapo, na una Uzima wa Milele. Mungu anaingia ndani yako.

³⁶⁶ Sasa tazama, Uzima wa Milele; Yesu alisema, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, na hataingia hukumuni bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Wewe ni kiumbe kipya papo

hapo. Kisha Paulo akawakuta baadhi ya watu hao, kule katika Matendo 19. Walikuwa na mhubiri aliyekuwa mwanasheria aliyeongoka, jina lake Apolo. Basi Apolo alijua sana Maandiko, naye alikuwa akithibitisha kwa Maandiko ya kwamba Yesu alikuwa ndiye Kristo. Ona?

³⁶⁷ Tazama sasa. Apolo, kwa Neno, alikuwa akithibitisha Neno. “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno. Yeye asikiaye Neno Langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele.” Mwafahamu? Apolo, kwa Neno, alikuwa akithibitisha. Nao hawa walikuwa Wakristo, walikuwa wafuasi, wanafunzi. Naye Apolo alikuwa akithibitisha kwa Neno, ya kwamba Yesu ndiye Kristo. Nao walikuwa na furaha kuu na wakapokea lile Neno, ingawa walijua tu ubatizo wa Yohana.

³⁶⁸ Basi Paulo alipopitia pwani za juu za Efeso, yeye akakutana na wanafunzi hawa na kusema, “Mlipokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?” Ona?

³⁶⁹ Naam unapoamini, Yesu alisema, “Una Uzima wa Milele.” Huko ndiko kuzaliwa mara ya pili. Ndiko huko kuongoka kwako, kugeuzwa. Basi Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni nguvu ya Mungu ambayo unabatizwa kwake na una ruhusa ya kutumia hizi karama tisa za kiroho zikitenda kazi kupitia kwako, kama kuhubiri, waijilisti, mitume, manabii, . . . na karama hizo zote za mwili ule zinaingia humu, unapobatizwa kuwa katika huu mwili. Na huko ni . . . hakukufanyi Mkristo zaidi, kunakuweka tu mahali pako kama roho ahudumuye katika Kanisa la Mungu aliye hai. Sasa mnafahamu? Ona?

³⁷⁰ Sasa swali ni . . . Hebu tuyajibu mfululizo, kuna maswali matatu.

“Katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja wa Kristo.”

Hilo ni sawa, 1 Wakorintho 12 itajibu hilo, vema.

“Tunapopokea kule kuzaliwa mara ya pili, je, hili hutendeka? Ni wakati huo?”

³⁷¹ Hilo ndilo wanalotaka kujua, naam. . . “Kwa Roho mmoja. . .” La. La. “Kwa Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja.” Ona, hapo sipo kuzaliwa mara ya pili kunapoanza, kuzaliwa mara ya pili kunaanza *unapomwamini* Bwana Yesu.

³⁷² Sasa ona, hakuna. . . hakuna jambo moja. . . Sasa sikiza. Ungefanyaje zaidi ya kuamini? Ungefanya nini tena? Ungefanya nini tena kuhusu hayo isipokuwa kuamini tu? Niambie jambo moja ungalitenda. Hakuna kitu uwezacho kufanya nje ya kuamini. Naam, kama kitu kingine cho chote kikitoka nje ya kuamini kwako, si tendo lako mwenyewe, ni tendo la Mungu. Hivyo basi. . .

³⁷³ Sasa kama tunganee kuwa unapo . . . Mara nyingi, nimeona, mara nyingi, watu wakikubali “thibitisho mathubuti la kunena kwa lugha” kuwa ni Roho Mtakatifu. Na wakati mwingine kuwatikisa watu, au kuwapiga-piga na kuwapapasa-papasa, wakisema, “Iseme. Iseme. Iseme. Iseme.” Mwajua, kurudia neno moja mara nyingi, “Iseme. Iseme. Iseme.” Ona, ni kitu fulani unachotenda wewe mwenyewe. Na—na—na haki . . . haki . . . ni—ni bure. Huenda ukapata mchafuko wa lugha. Huenda ukapata vitu vi—vingi mno, na miamsho. Bali kama kitu cho chote kikija nje ya imani yako binafsi, hapana budi ni kipawa cha Kiungu ambacho Mungu amekupa wewe. Ona?

³⁷⁴ Na katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja.” Hiyo ni sawa, ona. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni tendo tofauti na kuzaliwa mara ya pili. Moja ni kuzaliwa, nyingine ni ubatizo. Moja inakupa Uzima wa Milele, nyingine inakupa uweza. Inatoa uwezo wa kuingia katika Uzima wa Milele, ona, kutenda kazi. Sasa mmefahamu? Vema.

³⁷⁵ Sasa hapa mna lingine, la pili, bora sana la yale niliyokuwa nayo usiku ule:

61. Roho ya Yesu ilikuwa wapi katika hizo siku tatu mwili Wake ulipokuwa kaburini? Roho Yake ilikuwa wapi?

³⁷⁶ Sasa roho Yake iwapo utafuatilia Maandiko . . . Vema, tungepata tu mahali pengi. Lakini, nashangaa, nani ana Biblia? Ndugu Stricker, una Biblia? Vema. Ndugu Neville, unayo? Nifungulie Zaburi 16:10. Nani mwingine? Dada Wood, una Biblia pale? Vema, Ndugu Stricker, (Vema, mmoja wenu), wewe nifungulie Matendo 2:27, Matendo 2:27.

³⁷⁷ Basi sasa, kwanza, Yesu alipokufa, . . . Unapokufa, mwili wako hufa. Neno lile *mauti* maana yake ni “kutengana,” ni kutenganishwa tu na wapendwa wenu. Lakini hapa Yeye aweka hili katika Yohana Mt. sura ya 11, “Yeye alisikiaye . . .” Si . . . Samahani; hayo ni katika Yohana Mt. 5:24, “Yeye alisikiaye Neno Langu, yuna Uzima wa Milele.”

³⁷⁸ Yesu alimwambia Martha, aliyekuja kumlaki . . . Martha alisema, “Kama ungalikuwapo hapa, ndugu yangu hangalikufa. Lakini, hata sasa, yo yote utakayomwomba Mungu, Mungu atakupa.”

³⁷⁹ Yeye akasema, “Mimi ndimi ufufuo na Uzima.” Ona? “Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi; naye kila aishiye na kuniamini hatakuwa kabisa hata milele.”

³⁸⁰ Sasa—sasa, kuna sehemu yetu ambayo haifi. Na kama tu vile nilivyosoma mstari huo wa Maandiko, kila kilicho na mwanzo kina mwisho. Ila kisicho na mwanzo, hicho hakina mwisho. Kwa hivyo tunapomkubali Kristo, Mungu, tunakuwa wana wa kiume na wa kike wa Mungu, na Uzima wetu hauna mwisho kama tu wa Mungu usivyo na mwisho; tuna Umilele.

³⁸¹ Sasa neno *milele*, tumekwisha kulinena. Neno milele ni “*muda fulani*,” milele na (kiunganisho) milele. Nasi tuliona hapa ya kwamba ina—ina mwisho, kama tu vile maumivu yote, na magojwa yote, na huzuni yote, na adhabu yote, na kuzimu kwenyewe kuna mwisho.

³⁸² Bali Uzima wa Milele hauna mwisho, kwa maana haukuwa na mwanzo. Hauwezi kufa kwa sababu haukuzaliwa kamwe. Haukuwa kamwe na mwanzo wa siku zake, hauna mwisho wa wakati wake. Sasa, njia pekee tuwezayo kuishi Milele, ni kwa kupokea kitu fulani kilicho cha Milele. Na Mungu alikuweko, kusijakuweko kitu cho chote, Mungu alikuweko. Mungu hakuwa na mwanzo kamwe wala mwisho.

³⁸³ Basi Mungu alikuwa huyu Roho mkuu. Tulimfananisha Yeye na zile—zile rangi saba za upinde wa mvua unaofunika... Upinde bila shaka ungelifunika dunia kama haukuigusa dunia. Ni maji tu katika duara ya mpindo wa dunia, ndiyo yanayousababisha. Bali, sasa, kama vile Mungu alivyo wa Milele naye alikuwa Mkamilifu: amani kamilifu, furaha kamilifu, raha mstarehe. Hizo roho zote saba (kama tupatavyo katika Ufunuo), zilijidhihirisha wazi; zilikuwa Mungu, zikawa ukamilifu. Kitu chote nje ya hicho kimekuwa kitu kilichopotoshwa toka kwa Huo.

³⁸⁴ Basi njia pekee tuwezayo kufikia ikamilifu, ni kurudi tena kwa Huo (ukamilifu, ambao ni Mungu). Ndipo tunafikia ukamilifu, kisha tuna Uzima wa Milele; bila mwisho, wala bila—bila cho chote, ni daima Uzima wa Milele.

³⁸⁵ Sasa yeye ananena kuhusu nafsi... roho. Kwa maana sisi huilaza miili yetu mle kaburini, hata walio watakatifu sana kati yetu, kwa ajili ya mwili huu. Nao huo mwili... Kwanza, Mungu, yule Logos aliyetoka ndani ya Mungu...

³⁸⁶ Au kama tulivyoeleza, Wakatoliki wanauita, “uwana wa Milele wa Mungu.” Ambalo, kama nilivyosema hapo mbeleni, hilo neno hata halina maana. Ona, hakuwezi kuwepo mwana wa Milele, kwa sababu mwana hana budi kuwa na mwanzo. Na kwa hivyo Yesu alikuwa na mwanzo, Mungu hakuwa na mwanzo. Ona? Lakini Mwana alikuwa... si uwana wa Milele, bali Mwana aliyekuwa pamoja na Baba hapo mwanzo alikuwa Logos iliyotoka kwa Mungu.

³⁸⁷ Nayo ilikuwa mwili wa Kiungu wa Mungu uliotoka. Umbo la kibinadamu ambalo halikuwa na macho kama mnayoyaona; jicho bora. Halikuwa na maskio kama msikiavyo, bali kusikia kwa hali ya juu zaidi. Ona, ulikuwa ni mwili wa Kiungu, ambao, upinde huu wote wa mvua u—ulijidhili katika mwili huo wa Kiungu. Musa aliuona ulipopitia mwambani hivyo. Yeye aliona sehemu za nyuma, kasema, “Ulionekana kama wa mwanadamu.”

³⁸⁸ Ibrahimu alimwona Yeye alipoingia katika mwili wa kibinadamu na akala ndama, kanywa maziwa, akala siagi. Ibrahimu alimwona mara tu Yeye alipoingia, ndiposa, akatoweka papo hapo. Tuliona ya kwamba miili yetu imetengenezwa kwa vitu kumi na sita vya duniani, hivyo huunganishwa pamoja. Basi Mungu aliviunganisha, na akaingiza Malaika wawili katika miili hii; Malaika waliosimama na kuongea. Nao Malaika walikuwa wanadamu wakati mmoja . . . na kwa wakati huo.

³⁸⁹ Sasa tazama, tunaona ya kwamba, je, yule Melkizedeki alikuwa nani ila Mungu Binafsi! Hangalikuwa mwingine awaye yote, kwa kuwa Yeye alikuwa Mfalme wa Salemu—ambao ni Yerusalemu. Yeye hakuwa na baba wala mama, hangalikuwa Yesu, kwa sababu Yeye alikuwa na baba na mama. Huyu hakuwa na mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa maisha Yake; kunaye Mmoja pekee aliye na hayo, huyo ni Mungu. Ilikuwa ni Mungu akiishi hapa katika mwili wa Kiungu. Ona? Tazama, Mfalme wa Salemu.

³⁹⁰ Naam, Mungu ameishi katika nyakati zote, ndani ya watu wake. Mungu ndiye aliyekuwa ndani ya Daudi, aliyemfanya aketi juu ya mlima, na kama mfalme aliyekataliwa, na akalialia. Roho yule yule alidhihirishwa katika Yesu Mwana wa Daudi, aliyekataliwa, Yerusalemu, kisha akalialia.

³⁹¹ Yusufu, aliyeuzwa kwa vipande thelathini vya fedha, akachukiwa na ndugu take, akapendwa na baba yake, akaketi kwenye mkono wa kuume wa Farao, na hamna mtu angalimjia ila kwa ku . . . apitie kwa Yusufu, na baragumu ililia na kila goti likapigiwa Yusufu: mfano kamili wa Kristo. Huyu alikuwa ni Roho wa Kristo akiishi katika hao watu. Ona?

³⁹² Sasa, sasa hapa Yesu alipokufa, ilikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Mungu alifanyika mtu. Katika sheria za ukombozi, njia pekee ambayo mtu angalikomboza mali iliyopotea ya Israeli, ilimbidi yeye awe mtu wa jamaa. Ilimbidi awe mtu wa jamaa aliye karibu. Kitabu cha Ruthu kinaeleza vizuri sana; ni sharti awe mtu wa jamaa. Kwa hivyo ilimpasa Mungu awe wa jamaa ya mwanadamu, kusudi mwanadamu apate kuwa wa jamaa ya Mungu. Ona?

³⁹³ Yeye ana roho ndani yake, mwanadamu huwa nayo anapozaliwa, kwa sababu ni roho ya maumbile. Ni roho ya kilimwengu, ni roho wa—wa Mungu wa dunia hii. Yeye ni mzao wa Adamu tu.

³⁹⁴ Mti huzaa aina yake. Mimea huzaa aina yake. Wanyama huzaa aina yao. Wanadamu huzaa aina yao. Wao ni vitu vilivyotokana na vya asili. Mwafahamu?

³⁹⁵ Sasa, sasa mwanadamu anapozaliwa, yeye huzaliwa mwenye roho ya ulimwengu huu. Hiyo ndiyo sababu hana budi kuzaliwa mara ya pili. Kwa kuwa roho hii ilikuja kwa kuzaliwa na

baba na mama, ambao ulikuwa uzazi wa kujuana kimwili, na bila shaka haingeishi milele. Kwa hivyo sharti azaliwe mara ya pili. Na kabla hajafanya hivyo, ilimpasa Mungu kushuka na kumtengenezea njia ya kuzaliwa mara ya pili: kwa sababu yeye hakuwa na njia ya kujikomboa, hakuwa na tumaini. Hakuwa...bila tumaini, bila Mungu, bila Kristo ulimwenguni, amekwisha kupotea na kuangamia. Ha—ha... hamna cho chote angalifanya kujiokoa mwenyewe. Yeye... kila...Haijalishi kama yeye alikuwa ni kuhani mkuu, wala askofu, wala papa, hata awe nani, ana hatia tu kama mtu ye yote yule.

³⁹⁶ Kwa hivyo, ilihitajika Mmoja asiye na hatia, kuitenda. Na yule pekee ambaye hakuwa na hatia alikuwa ni Mungu Binafsi. Basi ilimpasa Mungu kushuka awe mwanadamu (naye akaja katika umbo la Kristo) kuzuia uchungu wa mauti, kuondoa uchungu wa mauti, kutukomboa, kusudi sisi...si kwa matendo yetu wala uzuri wetu (hatuna wo wote), bali kwa neema Yake, tupate kuokolewa. Ndipo tunapokea Uzima Wake katika huu mwili unaokufa, nasi sasa tu wana wa kiume na wa kike wa Mungu, na tuna Uzima wa Milele ndani yetu. Sisi tu wana wa kiume na wa kike wa Mungu. Hivyo basi, Yesu, akiwa hai...

³⁹⁷ Wala hakuna mwanadamu, haijalishi alivyo mwovu wala alivyo mzuri, anapo...anapoondoka duniani, yeye hajafa bado. Yuko mahali pengine. Bali ana uhai ambao utaangamia, baada ya kuadhibiwa kuzimuni kwa ajili ya matendo yake, yeye... inngawaje uhai huo hauna budi kukoma. Kunayo tu aina moja ya Uzima wa Milele.

³⁹⁸ Sasa, tumekwisha kueleza hayo. Kama mtu anaweza kuwa mwenye dhambi na kuadhibiwa milele...Hawezi kuadhibiwa milele ijapokuwa awe na Uzima wa Milele. Iwapo yuna Uzima wa Milele, basi ameokoka. Ona? Kwa hivyo kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, nayo ni Zoe, "Uzima wa Mungu." Naye hawezi kupotea.

³⁹⁹ Lakini waovu wako mahali pa—pa kungojea (katika mateso) hukumu yao (wahukumiwe kulingana na matendo yao waliyofanya katika miili yao) siku ya mwisho. Naam, lakini tuta...Dhambi za watu wengine huwatangulia, na za wengine huwafuata.

⁴⁰⁰ Basi tukiungama dhambi zetu, Yeye ni mwenye haki kutusamehe, hivyo basi, haitatubidi kamwe kusimama kwenye hukumu ya Mungu. Mwafahamu? Tazama, Warumi 8:1, "Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu." Walio katika Kristo. Waliopita toka mautini kuingia Uzimani; ona, hatuna hukumu ya adhabu na tulikuwa katika Kristo Yesu. "Wasioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho." Ona? "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa Milele."

401 Basi iwapo nimekubalika katika Kristo, na Kristo amechukua hukumu yangu, nami nilikubali upatanisho Wake kwa ajili ya dhambi zangu, Mungu awezaje kunihukumu? Yeye amekwisha kunihukumu, wakati alipomhukumu Kristo. Basi niko huru kwa hukumu. “Ndipo nitakapoona ile damu, nitapita juu yenu.” Ona?

402 Lakini, sasa, sivyo mwenye dhambi. Yeye huenda kwenye mateso. Nasi tunajua hilo ni kweli. Mwenye dhambi yu hai. Yuko kwenye mateso. Yuko mahali ambapo hajui... Hivyo ndivyo hawa wapandishao pepo na wapiga bao huita hizi roho za watu waliokufa, namna fulani ya mchezo na kufanya mzaha na kadhalika. Kama mmewahi kuona yo yote ya hayo. Vema, mbona? Wao hawa...

403 Mwone huyu Binti Pepper, kabla nakala yangu juu ya *Muujiiza wa Donny Morton* haijachapishwa. Wangapi walisoma nakala hiyo? Naam, wengi wenu mlisoma, bila shaka. Na yako kwenye gazeti la *Reader's Digest*. Mlitambua, kabla tu hiyo ya Binti Pepper haijachapishwa, yule mpandishaji pepo mashuhuri sana ulimwenguni uliyepata kumjua. Kurasa kumi na mbili zilitolewa kwa hadithi yake. Na kwa miaka hamsini... Wamempeleka kote ulimwenguni, na mathibitisho ya kisayansi na kadhalika, kuwa “yeye hakika huongea na wafu, na hao watu kujitokeza.” Nini? Jina la Mungu halikutajwa hata wakati mmoja, hamna toba, hamna uponyaji wa Kiungu, hamna lo lote kwake, ona.

404 Jambo pekee lililotendeka, ni wale watu waliotajwa, “Yohana, je, hunijui? Mimi ni George niliyekuwa mahali *fulani*, nami nilifanya *hivi* na *vile*. Je, unakumbuka mahali tulipoenda na kufanya hivi?” Ona, hayo tu ndiyo wajuayo. Wameangamia. Wamepita toka... Wao—wao hawana kitu kilichobakia ila hukumu.

405 Mti uegemeavyo, ndivyo uangukavyo. Na utakavyokufa... Hiyo ndiyo sababu sikubaliani na kuombea wafu, ona, kuombeana kwa maombi au—au ushirika wa Watakatifu na kadhalika. Haiwezekani kamwe, kulingana na Neno la Mungu. Haifai lo lote kumwomba ye yote baada ya wao kufa. Wameangamia. Wao wame... wame... wamekwisha kuvuka mpaka kati ya neema na hukumu. Au waliiondea neema, au wakaiacha neema. Yesu alisema hivyo, katika mlango wa 16 wa Mathayo Mt. Yeye—Yeye alilifundisha; sura ya 16 ya Marko, naamini ndipo ilipo. Yule tajiri na Lazaro; hamna mtu awezaye kuruka shimo hili kubwa, na hamna atakayewahi kuliruka. Naam, Ona? Hayo yatosha.

406 Basi bali Kristo alipokufa, kila kitu kilipaswa kushuhudia kwamba Yeye alikuwa Kristo. Sasa hebu tuliendee swali lako. Kwanza, nyota zilikataa kung’aa, jua likatua, mwezi haungetoa mwangaza wake, dunia ilikokomoa miamba yake, katika kufa

Kwake. Naye akaenda na kuwahubiri nafsi waliokaa kifungoni, ambao hawakutubu katika siku za uvumilivu wa siku za Nuhu. Yeye, iliwabidi wamtabue. Tazama hilo! Na kama kwa bahati kuna mwenye dhambi hapa usiku huu, wazo hilo kwa dakika moja hivi. Hivi karibuni Injili hii unayosikia ikihubiriwa hivi sasa, itakupasa uishuhudie. Mahali fulani utapiga goti lako, haijalishi u nani. Huenda ikawa miaka elfu kumi tangu leo, huenda isiwe hata . . . asubuhi. Iwe lini, utapiga magoti mahali fulani, nawe utasikia ukihubiriwa Injili ii hii.

⁴⁰⁷ Kwa maana baada ya roho hizo kuwa kifungoni, ambazo hazikutubu wakati Henoko na hao wote walipohubiri, na Nuhu. . . na kwa ule uvumilivu wa Mungu, kama ilivyo sasa, ukingoja wakati ule uje. Naye Nuhu na Henoko na kadhalika wote walihubiri, nao hao watu wakawacheka na kuwafanyia mzaha. Nao walikuwa kifungoni, kisha Yesu akaenda na kuwahubiri nafsi waliokaa kifungoni. Yeye akashuhudia! Mbingu zikashuhudia, “Yeye ndiye.” Dunia ikashuhudia, “Yaye ndiye!” Kuzimu kukashuhudia, “Yeye ndiye.”

⁴⁰⁸ Biblia ilisema kuwa ili. . . Daudi, miaka mingi iliyopita, katika Zaburi. . . Vema, Ndugu, sama Zaburi, tafadhali, Zaburi 16:10: [Ndugu Neville asoma, “Maana hutakuachia kuzimu nafsi yangu; wala hutamtoa Mtakatifu Wako aone uharibifu.”—Mh.]

⁴⁰⁹ Soma jambo lile lile ndugu, ambalo Petro alihubiri,, katika Matendo, sura ya 2, aya ya 27: [Ndugu Stricker asoma, “Kwa maana hutaichia roho yangu katika kuzimu: wala hutamtoa Mtakatifu Wako aone uharibifu.”—Mh.]

⁴¹⁰ Soma vifungu viwili hapo nyuma, ndugu, ili upate utangulizi—utangulizi wake: [Ndugu Stricker asoma, “Maana Daudi ataja habari Zake, Nalimwona Bwana mbele yangu siku zote, kwa kuwa yuko upande wa mkono wangu wa kuume, nisitikisike. Kwa hivyo moyo wangu ukapendezewa, ulimi wangu ukafurahi; tena mwili wangu nao utakaa katika matumaini. Kwa maana hutaichia roho yangu katika kuzimu; ala hutamwacha Mtakatifu wako aone uharibifu.”—Mh.]

⁴¹¹ Soma kifungu kinachofuata sasa: [Ndugu Stricker asoma, “Umenijulisha njia za uzima; utanijaza furaha kwa uso wako.”—Mh.]

⁴¹² Naam ona. Sasa, rafiki yangu wa Mashahidi wa Yehova, ningependa kukuuliza juu ya hilo. Ona? Kama kuzimu ni mahali. . . Jahanamu, Kuzimu, vyo vyote utakavyo kupaita; kama hayo hukomea kaburini, basi mbona Yeye akasema, “Kwa maana hutaichia roho Yangu katika kuzimu; wala hutamtoa Mtakatifu wako aone uharibifu?” Basi, na hayo je? Ona?

⁴¹³ Ndio huu mwili Wake, kaburini; na nafsi yake ilikuwa kuzimuni, akihubiri, hai! Na hilo je? Yeye alikuwa tena katika mwili Wake wa Kiungu. Nafsi Yake ilikuwa kule chini pamoja na watu hao waliokuwa pia katika mwili wao wa Kiungu pia.

Na alikuwa akiwashuhudia, kuwa wao “hawakutubu katika ule uvumilivu.”

414 Yeye... Yaani, Yeye alibisha mlangoni. Na mlango ulipofunguliwa, na nafsi hao wote waliotubu, Yeye akasema, “Mimi ni yule Mzao wa mwanamke. Mimi ndiye ambaye Henoko hapa...” Kule Paradiso, mahali pengine. Usipasahau mahali hapo patatu, sasa: mahali pa waovu, mahali pa wenye haki, na kuzimu kwenyewe. Ona?

415 Ni kama tu utatu wa Mbinguni, kama: Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu. Kama tu utatu wa yule mnyama: yule nabii wa uongo, yule mnyama, na ile—ile chapa ya mnyama. Na hivyo vyote, kumbuka, vyote viko katika utatu. Utatu hufanya mmoja, kukamilishwa. Moja imekamiliwa. Wewe umekamilika, mmoja katika tatu: nafsi, mwili na roho: maji, damu, na neva. Ona, hata uwe nani, sharti uchukue tatu kusudi upate kilicho kikamilifu. Chukua kioo chenye pembe tatu na upitishe jua ndani yake, unapata upinde mkamilifu wa mvua. Ona, kila kitu, sharti uwe na tatu kukamilisha.

416 Basi sasa, kumbukeni hilo, Yeye alipokufa, alikwenda kwanza na kuwahubiri kwanza nafsi ambao hawakuwa kifungoni... waliokuwa kifungoni, akashuhudia kuwa ni “Mzao wa mwanamke.” Alikuwa “Yeye Yule Henoko aliyemwona akija na elfu kumi za watakatifu Wake.” Yeye alipaswa kushuhudia Maandiko yaliyohubiriwa na Nuhu, na Henoko, na wale wenye haki, kuwa “Yeye alikuwa ndiye Yule.” Kila kitu kilipaswa kulitambua!

417 Kisha akashuka hata kuzimuni na kupokea fungo za mauti na kuzimu toka kwa Shetani.

418 Akarudi Paradiso; naye akawaleta Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, na hao wenye haki; akawafufua (Mathayo 27), nao wakatoka makaburini na kuingia mjini, na wakawatokea watu barabarani. Haleluia! Naam!

419 Naam, bali mwili Wake... Nafsi Yake ilipokuwa humu ikiwashuhudia waliopotea, humu chini akichukua zile funguo toka kwa Shetani, huku akirudi akiwaleta Ibrahimu, na Isaka; nafsi Yake ilikuwa imelala mle... Nafsi Yake ilikuwa chini kule ikitenda hayo, na mwili Wake ulikuwa umelala kaburini. Hiyo ndiyo sababu Yesu alisema... Watu husema, “Vema, mbona Yesu asema, ‘Siku tatu, nitaufufua—siku tatu nitaufufuka?’ A—alikufa Ijumaa adhuhuri, akafufuka Jumapili asubuhi.”

420 Lakini tazama, ilikuwa ni “katika siku tatu,” kama ungechukua ile kamusi. Kwa kuwa Yeye alijua kuwa Daudi, chini ya upako (ya upako wa Roho Mtakatifu), alisema, “Sitamtoa Mtakatifu wangu aone uharibifu.” Yeye alijua hilo lilimhusu Yeye. Alijua hayo yalimaanisha Yeye binafsi. Yeye alikuwa ndiye Mtakatifu wa Mungu, naye alijua kuwa uharibifu huingia katika

masaa sabini na mawili. Mahali fulani katika hizo siku tatu, Yeye angetoka mle tena, kwa maana Maandiko hayawezi kutanguka.

421 Na kila ahadi ndani Mle inanihusu mimi na inakuhusu wewe, ni yetu.

422 Yeye alisema, “Uvunjeni mwili huu, nami nitaufufua katika siku tatu.” Kwa kuwa, hata alisema, “Sitakuachia kuzimu nafsi Yangu, wala sitamtoa Mtakatifu Wangu aone uharibifu.”

423 Yeye alijua, katika siku tatu mwili huo ungetoka mle. Yeye hakukaa zile siku tatu zote. La, bwana, bila shaka hakuzimaliza. Alikaa tu tangu Ijumaa jioni hata Jumapili asubuhi, si hata chembechembe moja ingeliona uharibifu.

424 Naye alikuwa amekufa, na kutiwa dawa asioze, na alikuwa amelala...au amezongwa-zongwa katika sanda, na kulazwa kaburini. Katika nchi hiyo yenye joto na zimwi, angechukua tu masaa machache kuharibika. Inakupasa ku...kuzimba, mwajua, mwili wake, pua lake linatokomea na kadhalika, uharibifu unaingia; hiyo nchi yenye joto na unyevu. Na ungeliharibika, kwa sababu ulikuwa mwili. Lakini Yeye alijua, kabla hiyo chembechembe hai haiharibika, Mungu alisema kwa nabii Daudi, “Sitamtoa Mtakatifu Wangu aone uharibifu.”

425 Jinsi Yeye alivyochukua Neno la Mungu na kuishi kwalo! Sasa, kila moja ya ahadi hizo ndani humo zinazomhusu, Mungu alitimiza kila moja yazo. Na kila ahadi zinazomhusu mwamini, Mungu atatimiza kila moja yazo. Amina. Usitie shaka. Amina. Basi, nafsi Yake. . .

Je, unafikiri ni . . . La, samahani. Roho ya Yesu ilikuwa wapi katika hizo siku tatu Mwili Wake ulipokuwa kaburini?

426 Roho Yake ilikuwa jehanum, kuzimuni; naye akafufuka. Na huenda nikaongeza kutaja jambo ndo—ndogo hapa ambalo lingewasaidia sana. Alipofufuka, Yeye...Alipofufuka katika wafu, bila shaka alikuwa bado hajamaliza kazi ya ukombozi. Naam. Ilimpasa kusafisha kitu hicho chote. Ile deni ilikuwa imelipwa, bali ile hofu ya kuzimu, ile hofu ya kaburi...Na hapa, Yeye alipo—alipokufa aliendelea. Hakukoma kufanya kazi alipokufa, aliendelea kuhubiri!...?...Kunradhi kwa kukosa kiasi, nafikiri, Bali hakukoma kamwe!

427 Hutakoma! Mwili wako huenda ukapumzika kidogo, lakini Mungu ataufufua, Yeye aliahidi angefanya hivyo. Lakini hutaangamia kamwe, jinsi Mungu asivyoweza kuangamia. Naam. Tazama, Kwake...baada ya kufa Kwake, jinsi...kufa kulingana na wanafunzi. Yeye alikuwa amelala, jinsi alivyokuwa. Walimfanya alale; kama alivyosema kuhusu Lazaro, “Nitakwenda kumwamsha.” Ilimpasa Mungu kumwamsha.

428 Tazama, alishuka chini kabisa, akaendelea kuhubiri. Naye akawahubiri nafsi waliokaa humu kifungoni. Akaondoka akaenda moja kwa moja hata kuzimuni, akamnyang'anya

Shetani zile funguo. Akarudi tena na kuhubiri katika paradiso, kisha akafufuka siku ya tatu. Akawazuru mitume Wake kwa siku arobaini, kisha katika mwisho wa siku ya arobaini, akapaa juu; kwa sababu kila kitu juu yetu, ushirikina na kadhalika. . . Yeye aliondoa kila ushirika, kila shaka, na kutungisha mstari wa maombi toka duniani hata Utukufuni katika kupaa Kwake. Alipaa juu na kuketi mkononi mwa kuume mwa Utukufu Wake. Mshindi! Yule Mshindi Mkuu, bila shaka. Mauti hayangalimzuia! Kuzimu hakungalimzuia! Dunia haingemzuia!

⁴²⁹ Alipokuwa hapa duniani, Yeye alipewa. . . Yeye alikwenda kwenye mji ulio chini sana na kwa watu walio chini sana, na akapewa jina la chini sana. Hayo ndiyo watu walimtendea. Alikwenda Yeriko, mji ulio chini sana. Mtu aliyekuwa mfupi sana ilimpasa kupanda juu ya mti akamwamgalie. Hapo ndipo mwanadamu alipomweka. Yeye alikuwa anayetawadha miguu, kazi mbaya sana ambayo ingalitolewa. Akawa mtu wa chini sana. Naye alipewa jina la chini zaidi ambalo lingeweza kutolewa, *Beelzebuli*, “mfalme wa pepo.” Mwanadamu alimpa jina la chini sana, mahali pa chini sana, na kumpeleka Yeye mahali pa chini sana katika kuzimu ya chini sana.

⁴³⁰ Mungu alimfufua na kumpeleka katika Mbingu za Juu sana, na Jina lipitalo kila jina. Haleluiya! Naam, ilimpasa kutazama chini, kuona Mbinguni. Kiti Chako kimewekwa juu ya mbingu za Mbinguni. Na Jina kuu sana lililowahi kutajwa Mbinguni na duniani linapaswa kuwa. . . linamzunguka Yeye. Hayo ndiyo Mungu alimtendea. Mwanadamu alimweka chini sana, naye Mungu akamwinua juu sana. Ndiye huyo, toka palipo chini sana hata palipo Juu sana.

⁴³¹ Yeye akawa wa chini sana kusudi atupandishe Juu sana. Yeye akawa sisi, kusudi sisi kwa neema Yake tuweze kuwa Yeye, wana wa Mungu. Hapo ndipo alipokwenda. Amina! Jina Lake lihimidiwe. Yeye alitengeneza njia tupate kuja, pia, wakati mmoja, “Kwa sababu Mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai.”

⁴³² Jamani si ajabu. . . Mtu anapopata hilo ono, hamna mtu awezaye kulieleza. Hata nao pia wamejaribu kulieleza, wakarukwa na akili; huu wimbo mkuu: “*Ee upendo wa Mungu, ni wa dhamini na msafi vipi; haupimiki na una nguvu sana.*” Hicho kifungu cha mwisho. . . au naamini kifungu cha kwanza ni: “*Kama tungaliijaza bahari kwa wino, Na anga tukaliunda kwa karatasi; . . .*” Mwajua huo ulitoka wapi? Uliandikwa kwenye wenda wazimu. . . ukutani mwa hospitali ya wenda wazimu. Hamna mtu awezaye kamwe kuueleza huo Upendo wa Mungu. Ee, hayasemeku, yale aliyotufanyia. Jamani, ungewezaje kuweka angaa fadhili moja mle? Ni neema Yake, tangu mwanzo hata mwisho. Nilikuwa nimepotea, nimekwisha, mdhaifu, si mwema, nilikuwa bure, kisha Yeye kwa neema Yake akaja na kutuokoa sisi. Ee, jamani. Hiyo ni. . . Huyo ndiye Bwana wangu. Huo ni upendo Wake, huo ni wema Wake.

433 Sasa tuna dakika saba hivi na karibu maswali kumi na matano.

62. Je, unafikiri ni sawa kwa wanawake kufanya kazi ya kibinafsi nje ya kanisa?

434 Naam. Hilo ni swali tu, ni...si swali la Kimaandiko, lakini...Bila shaka, nafikiri ni sawa. Naam, bwana, sisi sote tu watenda kazi pamoja. Wanawake wana mahali pao, na bila shaka wanapo. Naam, bwana. Fanya kazi yo yote tu ya kibinafsi uwezayo kufanya, na Mungu atakubariki kwa kufanya hivyo.

Vema, sasa hebu tuone:

63. Tafadhali eleza utatu. Mwana awezaje kuketi kwenye mkono wa kuume wa Baba, akituombea...kwa Baba, kama kama wao si nafsi mbili?

435 Vema, rafiki mpendwa, hilo ni...huo ni—huo ni ufunuo. Kama Yesu alisema, “Mimi na Baba Yangu ni mmoja,” basi wao wawezaje kuwa wawili? Ona? Sasa, wao si wawili.

436 Mwanamke mmoja siku moja aliniambia, nami nilikuwa nikieleza hilo, alisema, “Wewe na mke wako ni—ni wawili, bali mu mmoja.”

437 Nikasema, “Lakini Mungu na Mwana ni tofauti na huo, ona.” Nikasema “Waniona mimi?”

“Naam.”

“Je, unamwona mke wangu?”

“La.”

438 Nikasema, “Basi, Baba na Mwana ni tofauti; Yesu alisema, “Unionapo Mimi, umemwona Baba.” Ona?

439 Baba na Mwana...Baba alikuwa Yehova Mwenyezi (Mungu) akiishi katika maskani yaliyoitwa Yesu Kristo, aliyekuwa Mwana mpakwa mafuta wa Mungu. Yesu alikuwa Mwanadamu, Mungu ni Roho. Na hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote, ila Mwana pekee wa Baba amemtangaza. Yeye alikuwa... Yeye...Nafsi Yake, utu Wake, Uungu Wake, vyo vyote Yeye alivyokuwa, Yeye alikuwa Mungu! Yeye hakuwa cho chote chini ya Mungu wala cho chote zaidi Yake. Ingawaje, Yeye alikuwa mwanadamu. Alikuwa mwanadamu, nyumba alimoishi Mungu. Naam, Yeye alikuwa maskani ya Mungu.

440 Sasa, iwapo unataka Maandiko juu ya hilo...Ndugu Neville, nifungulie Marko Mt. 14:32. Nawe Dada Wood, nifungulie Waefeso 1:20. Mtu mwingine aliye na Biblia? Vema, inua mkono wako. Dada Arnold, unayo nyuma kule? Vema, nifungulie Matendo 7:55. Vema. Marko 14:62, Ndugu Neville; na Dada Wood ni Waefeso 1:20; Matendo 7:55, Dada Arnold.

441 Vema, umeipata Ndugu Neville? Vema, sasa soma; [Ndugu Neville asome, “Na Yesu akasema, Mimi ndiye, nanyi mtamwona

Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija na mawingu ya mbinguni.”—Mh.]

442 Vema, basi, tazama fungu la kwanza la maneno haya, Yesu alisema, “MIMI NDIYE.”

443 “MIMI NDIYE.” Nani alikuwa MIMI NDIYE? Hapajakuwepo mtu duniani ambaye angeifafanua. Hata... ninyi msomao kamusi na kadhalika, hakujawahi kuwa na mwanadamu ambaye angeifafanua...Ni j-v-h-u. Na hata wanavyuoni wa Kiibrania hawangelitamka kamwe. Kile kijiti kilichowaka moto pale, siku ile Yeye alipokutana na Musa, ilikuwa j-v-h-u. Kwa hivyo walilitamka “j-o-h, Jehovah,” lakini si “Jehovah.” y-v-h-u, ona, hakuna ye yote alijuaye.

444 Nanyi mwasema, “Vema, Musa hakulifahamu.”

445 Yeye alisema, “Nitasema ni nani?”

446 Yeye alisema, “Sema, “MIMI NDIYE” alikutuma. MIMI NDIYE.”

447 Sasa tazama. MIMI NDIYE ni mtajo wa wakati uliopo, si “niliyekuwako” au “nitakayekuwako,” MIMI NDIYE.” Naam, Yeye alisema, “Hili litakuwa ukumbusho kwa vizazi vyote: MIMI NDIYE.”

448 Sasa mtazame Yesu hapo karamuni siku hiyo. Hao walisema, “Tunajua sasa una kichaa.” Maneno yanayofaa, “Una wazimu (*wazimu* ni “kichaa”). “Tunajua wewe una kichaa. Wewe u Msamaria, nawe una pepo.” (Yohana Mt. sura ya 8) Naye akasema, “Sasa, unasema u...umemwona Ibrahimu, nawe ni mtu asiypata miaka hamsini?” (Huenda Yeye alionekana kuwa mzee zaidi ya umri Wake, lakini alikuwa tu na miaka thelathini, bali kazi Yake...) Kasema, “Unataka kusema kuwa hujapita umri wa miaka hamsini, na unasema umekwisha ‘kumwona Ibrahimu’? Tumeng’amua Ya kuwa una kichaa sasa.” Ona?

Akasema, “Yeye Ibrahimu asijakuweko, MIMI NIKO.”

449 “MIMI NIKO,” Yeye alikuwa MIMI NIKO aliye mkuu. Hapa Yeye anawaambia Wayahudi hawa tena, ona, “MIMI NIKO! Nanyi mtakaponiona Mimi nikija kwenye mkono wa kuume wa nguvu.” Sivyote?

450 Soma hilo tena ndugu. [Ndugu Neville asoma “Nanyi mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija na mawingu ya mbinguni.”—Mh.]

451 Soma yako sasa, Dada Wood: [Dada Wood asoma, Waefeso 1:20—Mh.] Naam, mama. [Dada Wood asoma, “Aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho”—Mh.]

452 Vema, soma yako, dada. Ona, ni yale yale tu: [Dada Arnold asoma, “Lakini yeye akijaa Roho Mtakatifu, akakaza macho

yake, akitazama mbinguni, akauona utukufu wa Mungu, na Yesu akisimama mkono wa kuume wa Mungu.”—Mh.]

453 Sasa, mwaona, Mungu hangekuwa na mkono mkubwa wa kuume, ona, na Yesu akisimama upande wa mkono wa kuume. *Mkono wa kuume* maana yake ni “mamlaka.” Ona? Kwa mfano, vipi kama—kama ningalikuwa na mamlaka yote juu ya kanisa, au nilikuwa askofu, na Ndugu Neville akapachukua mahali pangu, yeye angekuwa mkono wangu wa kuume. Ona, hilo lamaanisha kuwa yeye ana...yeye angekuwa mkono wangu wa kuume.

454 Sasa, Yesu yuko upande wa kuume wa Nguvu. Naam, Yeye asema hivyo, hapa katika Waefeso, anapolieleza, “Yeye yuko mkono wa kuume wa Nguvu.” Mamlaka yote juu ya Mbingu na nchi “—(Yeye alisema, baada ya kufufuka Kwake) “nimepewa Mimi. Nina mamlaka yote juu ya Mbingu na nchi. Enendeni basi mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, mkiwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, Mimi niko pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.”

455 “Mamlaka yote juu ya Mbingu na nchi.” Yako wapi... Kama kuna Mungu mwingine isipokuwa Yeye, huyo hana mamlaka. Ona, hamna Mungu mwingine. “Mamlaka yote juu ya Mbingu na nchi” yamo mkononi Mwake. Kwa hivyo, mwaona, “Yeye amesimama katika mkono wa kuume,” (kama huyo mtu alivyouliza lile swali), haimaanishi. . .

456 Sasa tazama! Ule mwili... Mungu ni Roho. Naam, wangapi wanafahamu hilo? Semeneni “Amina.” Mungu ni Roho, Yesu ni Mwanadamu, basi Yesu alikuwa Mungu aliyefanyika mwili. Yesu alikuwa... Hatungemwona Mungu kamwe, ona, Yeye ni Roho. Huwezi kuona roho. “Hakuna mtu aliyemwona Mungu kwa wakati wo wote.” Hamna mtu hangalimwona Mungu.

457 Basi hebu niseme hili, “Ninyi nanyi hamjaniona bado.” Hamjawahi kuniona maishani mwenu mwote, hamtaniona kamwe. Naam. Mmeuona mwili huu unaomfunua mtu huyu aliye hapa sasa. Naam, mwili huu hauna Uzima wa Milele, bali roho ina Uzima wa Milele. Mwili huu utarudi, bali utajitokeza tena katika mfano wake, kama tu jinsi puje ya ngano iingavyo ardhini. Msingi wa Kikristo umo katika ufufuo, si kurudisha hali. Ufufuo; Yesu yule yule aliyekufa, ndiye Yesu yule yule aliyerudi. Ukifa ukiwa na nywele nyekundu, utafufuka mwenye nywele nyeusi. Ona, ni ufufuo.

458 Unapokula... Nilimuuliza daktari hilo, si muda mrefu umepita, nilisema, “Mbona nilipokuwa na umri wa miaka kumi na sita... Kila nilipokula, niliyaimarisha maisha yangu?”

459 Kasema, “Naam.”

460 Unaingiza chembechembe hai mpya—mpya kila unapokula...mwili hufanya...au chakula hufanya

chembechembe hai za damu, nayo hiyo chembechembe hai ya damu inakufanya upate nguvu zaidi. Hivyo ndivyo unavyoishi. Basi, kitu fulani hakina budi kufa kila mara, ili upate kuishi. Kila siku, kitu fulani hufa: ukila nyama, ng'ombe alikufa, au cho chote ulacho; na samaki alikufa; au ile—au ngano ilikufa, kufanya mkate; kiazizi kilikufa, kilichofanya vile viazi; na ile . . . kila aina ya uhai; waweza kuishi tu kwa vitu vilivyokufa.

⁴⁶¹ Nanyi mwaweza kuishi milele kwa sababu kitu fulani kilikufa, Yesu. Si kwa sababu ulijiunga na kanisa, si kwa sababu ulibatizwa, si kwa sababu ulikiri Ukristo; kwa sababu ulikubali Uzima wa Yesu Kristo uliomwagwa . . . damu iliyomwagwa kwa ajili yako, na ukamkubali kama Mwokozi wako binafsi.

⁴⁶² Sasa, tazama, nauliza hili. Nataka kuwaulizeni ninyi hili. Tazama hili, ni zuri mno. Labda nimekwisha kulifundisha hapo mbeleni (sijui) hapa; ukihubiri kila mahali, unasahau uliyosema mahali . . . mahali fulani. Lakini, mbona, basi . . .

⁴⁶³ Basi nadhani, Dada Smith . . . Sijui kama nilimjua Ndugu Fleeman kule nyuma au la. Na Tryphena, namkumbuka alipokuwa msichana mdogo. Wanikumbuka, nilipokuwa niki . . . nilipokuwa mdogo, mfupi . . . mwenye maungo manene; mweusi, nywele za ukoka. Nilikuwa mwana ndondi. Ee, nilifikiri mimi ni stadi sana duniani. “Ee,” niliwaza, “hakuna ye yote angelinishinda. La, bwana.” Lakini nili—nilijidanganya kwa hilo, mwaona. Lakini nili . . . sasa, niliwaza tu, “Jamani.” Nilidhani, “Kama ungeweka kitu hiki mgongoni mwangu, ningekibebe barabarani.” Hakika, sikujali kitu. Na kila nilipokula, nikawa mnene na mwenye nguvu wakati wote. Kila wakati niliongeza maisha mapya . . . Nilikula kabichi, viazi, na maharagwe, na nyama, kama tu nifanyavyo sasa. Nami nikapata nguvu na kuwa mnene wakati wote. Wala nilipofika yapata umri wa miaka ishirini na mitano . . .

⁴⁶⁴ Nakula vizuri zaidi sasa kuliko nilivyokula wakati huo, nyote mwanijua, mwajua hilo. Naweza hivyo. Lakini, mbona hivyo, Ndugu Eagen, basi, kama ninakula vizuri zaidi, zaidi yacho, vitamini bora, na kadhalika . . . Na kadiri ninavyokula, ndivyo ninavyofikia polepole. Na sasa ninafikia kuwa mtu mwenye mabega yaliyojikunyata, mwenye upara, na mvi, na mikono inakujamana, uso unarudi ndani, mabega yanainama, asubuhi ni shida kuamka, na . . . Jamani. Mbona hivyo? Ikiwa mimi huimarisha maisha yangu kila wakati nilapo, mbona hivyo basi?

⁴⁶⁵ Kama ninamimina maji katika gilasi kutoka kwenye jagi, na inajaa nusu, ndiposa inanza kupungua daima badala ya kujaa; na kadiri ninavyoimiminia ndivyo inavyozidi kupungua. Basi. Na hungaliithibitisha kisayansi hata kama ungalilazimika. Kitabu hiki ndicho kitu pekee cha kuthibitisha kuwa Mungu amekusudia; ni kukusudiwa, Mungu alituona tukija.

466 Ninyi wazee, wanaume kwa wanawake, labda baadhi ya waume ze—zenu na wake zenu wameaga dunia. Hilo hali—si hoja. Haleluiya. Wako tu ng'ambo ya pazia kule, wakingoja; bila shaka. Nao wana hamu ya kuwa pamoja nanyi tena. Naam, bila shaka, wanayo. Wana hamu ya kuwa pamoja nanyi tena. Biblia ilisema wanangoja, zile roho chini ya madhabahu zikilia, “Bwana, hata lini?” Ona? Hazimo katika hali yao halisi.

467 Mungu hakutufanya sisi Malaika, wanawake. Tutakuwa wanaume na wanawake daima, kwa sababu sisi ni uza—uzao wa maarifa ya Mungu Mwenyewe. Kila mara tunaweza kuwa wanaume na wanawake.

468 Lakini hayo yanasababishwa na nini? Ona, labda unadhani kuwa uliposhuka kwenda mimbarani, wewe na mumeo, mlisema tunaoana sisi kuwa mke wa ndoa na kuishi pamoja katika hali takatifu ya ndoa hii, na zile—zile neema za Mungu na kadhalika na kutoa ushuhuda wenu wote, na kuweka nadhiri. Muda si muda, mnaanza kuona mambo, nyote wawili. Yeye alikuwa wima, na nywele zake zilimetameta; na mama macho mazuri, macho madogo ya kahawia, au macho ya samawati, au cho chote kile. Jamani, jinsi ulivyomtazama. Ukatoka nje, ukamtazama baba, “Naam, yale mabega yamenyoka vilivyo”; na hatimaye yanaanza kujikunyata. Mama atakuwa na mvi, ataugua yabisi kavu na kadhalika. Muda si muda, ameondoka, ama ameaga dunia.

469 Ilikuwa nini? Mungu alipokuona umesimama pale, Yeye alisema, “Naam, hivyo ndivyo nikutakavyo.” Vema, kifo, njoo, ila hauwezi kuwachukua hata nitakapokuruhusu.

470 Jamani, nawaza ya Ayubu. Naam, Mungu alikuwa akitazama chini, Ayubu alijua Mungu alimpenda. (Na tazama, yeye hawezi kukuchukua.) Yeye alisema, “Unaye mikononi mwako, lakini usichukue uhai wake.”

471 Basi muda si muda, mabega yanaanza kujikunyata, na baadaye umeaga dunia. Nini ilitendeka?

472 Naam, katika ufufuo hakutakuwa na kitu hata kimoja kinachoonyesha mauti. Hakuwezi kuweco na cho chote kinachoonyesha dunia hii, cha yale. . . Ona, ulikuwa ukikua kwa mapenzi ya Mungu, ulikuwa na uhai. Kisha kifo kikakwingilia, kikakushusha. Huku unakula chakula kile kile na kadhalika, unakunywa maji yale yale, kila kitu; bali mauti iliingia. Bali picha imekwisha kuwekwa. Haleluiya. Katika ufufuo utaishi tena. Na hakutakuwa na mauti tena, wala mfano wa mauti, wala uzee, wala kilema, wala cho chote kile. Wasiokufa, tutakuwa katika mfano Wake, tumekamilishwa milele. Haleluiya. Ee, ni. . . Hilo lingemfanya kila mtu apige kelele, hasa unapofika umri wangu.

473 Umri wangu ni, nafikiri, ukiwazia, mwingi kuliko wakati mwingine wo wote. Uko tu kwa wakati huo wa kugeuzwa,

mwaona. Na...Unaanza kushangaa, “Haya yote ni nini? Nimefanya nini?” Natazama nyuma humu, nadhani, “Lo, rehema; vema, amekwenda wapi, Bwana? Mimi hapa, umri wa miaka arobaini na minane. Miaka miwili zaidi, nitakuwa nusu mia. Whiu. Mimi niko tu...”

474 Hebu tazama tu zile nafsi chache ambazo nimezileta. Nataka kuleta mamilioni na mamilioni zaidi. Mungu, nisaidie. Naona haya hata kuja nyumbani kwa likizo. Wazia, “Ee, mavuno yako tayari, na watenda kazi ni wachache. Mamilioni dhambini na aibuni wanakufa kila siku, sikiza wito wao.” Naondoka kwenda kitandani usiku na kusikia maskini makafiri wakipiga mayowe kule nchini. Jinsi wanavyokuja kwa mamia, wakinivuta mimi, na—na wakisimama nje pale kwenye uwanja wa ndege ambapo iliwabidi kuwapeleka askari pale kuwazuia, kusudi tu wasikie hadithi ya Yesu Kristo.

475 Na hapa twaweza kuwambebeleza, na kutangaza magazetini na kadhalika, na kupata mahali pazuri sana kwao kuketi chini, kawajumuisha sana kwa uimbaji bora, watakuja na “Oooh, vema, nafikiri hayo ni sawa, ingawaje, si ya dhehebu langu.”

476 Kisha kaondoka...“Jamani,” nilidhani, “ya—yaweza kudumu kwa muda gani?” Si...si halali. Na hapa tumetupa mabilioni ya matani ya chakula katika mapipa, na watu hao wangekipokea kwa furaha. Nao ni viumbe wa duniani kama tulivyo sisi. Lo, sisi...Vema, hilo haliwezi kudumu hivyo zaidi sana.

477 Vema, sasa, Baba ni nani? Baba na Mwana ni mmoja. Tazama, katika 1 Yohana 5:7 ilisema, “Wako watatu washuhudia Mbinguni, Baba, Neno (ambalo ni Mwana)... Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu; hawa watatu ni mmoja.”

478 “Wako watatu washuhudia duniani, ambao ni maji, damu, na Roho.” Hivyo ndivyo vitu vitatu vilivyotoka katika mwili wa Kristo. Walimchoma mkuki ubavuni: maji yakatoka, Damu ikatoka, “Katika mkono Wako naiweka Roho Yangu.” Naam, hivyo ni vitu vitatu. Hivyo vitatu si kimoja, bali *hupatana* kwa habari moja.

479 Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu; 1 Yohana 5:7, inasema, “Hawa watatu *ni* Mmoja.”

480 “Maji, damu, na Roho *hupatana* kwa habari moja.” Si moja, ila *hupatana* kwa habari moja. Kwa hivyo Baba...Na jambo pekee ambalo mwili ungefanya, Mungu anapoweza kujiona Mwenyewe, kwamba kwa adhabu uliyopewa mwili huu, kuna upata...kupati papo hapo, mwaona. Hapo ni wakati Yeye anapooni hiyo Damu imesimama kati Yake na hukumu. Ndilo hilo Neno Lake, kasema, “Siku utakapokula, utakufa.” Na hapo Yesu alisema, “Mimi...Lakini nilipachukua mahali pao. Ona nalichukua mahali pao.”

481 Kumbuka hadithi yangu usiku uliopita ambapo niliona lile ono la mwanamke mbaya sana aliyekuwa mle chumbani? Nami nilikuwa namhukumu, nikisema, “Mungu, mbona usipaangamize mahali hapa?” Ndipo Yeye akanionyesha *mimi* binafsi, ona. Basi nalimwendea mwanamke huyo na kumwambia yaliyotendeka. Basi, hili ndilo swali langu la mwisho.

64. Je, unafikiri, kulingana na Maandiko, kuwa Wayahudi wata . . . watamtambua Kristo kabla tu ya kule kunyakuliwa kwa Kanisa?

482 Na—na—naamini hasa kwamba kunyakuliwa kwa Kanisa . . . Hili ni wazo langu mwenyewe, ona. Na kama tungalikuwa na wakati, tungeliyachambua, lakini saa tatu i—imepita sasa. Tazama, naamini ya kwamba Wayahudi watampokea Kristo katika kule kuja Kwake kwa pili. Sasa kumbukeni, ili mtu yule ajue hili, macho yetu yalipofushwa . . . au macho yao yalipofushwa kusudi sisi tupate kuona. Kila mtu anajua Maandiko yanena hayo. Sivyo? Paulo anatwambia ya kwamba sisi . . . ya kwamba tulipofushwa . . . kwamba Wayahudi walipofushwa kusudi tupate kumpokea Kristo. Ona? Nasi ni mzeituni mwitu uliopandikizwa kwa kufanywa sehemu ya huo mti.

483 Basi maoni yangu ndiyo haya, nitawapeni tu . . . Wananiuliza, “Je, unafikiri . . . ?” Basi, nafikiri itakuwa hivi. Sijui. Hata iwe vipi, nina hakika kuwa kwa neema ya Mungu na rehema Zake, tutakuwa huko; ona, kwa neema Yake, hata iwe vipi. Huenda nisiweze kuyawazia, bali naona hivi. Naamini tuko katika wakati wa mwisho. Naamini wakati wa Mataifa uko unaisha hivi sasa. Naamini tuko mwishoni.

484 Na sasa Wayahudi; hapa pana vitu viwili ambavyo daima vimewaundi Wayahudi: Wamekuwa vipofu, hawangalionga; na kwa kuwa Mataifa, kwanza, wakati mwingi . . .

485 Niliongea na Myahudi kule Benton Harbor, Dada Smith, na unajua alivyoniambia? (hapa kwa mojawapo wa Waisraeli . . . mahali pa Waisraeli pale) Swali hili kuhusu kuponywa kwa yule mwanamke kipofu. Naye alisema, “Hamwezi mkamkata-kata Myahudi katika . . . Hamwezi mkamkata-kata Mungu katika vipande vitatu mkampa Myahudi; mkamfanya Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.” Kasema, “Huwezi ukamfanyia hilo Myahudi, sisi waabudu sanamu?” Kasema, “Tunaamini katika Mungu *mmoja*.” Ona?

486 Na mnapomfanya Mungu kuwa watatu: Mungu Baba, Mungu Mwana, Mungu Roho Mtakatifu; bila shaka mnapofusha Myahudi papo hapo, kwa sababu yeye anajua bora zaidi. Yeye anafahamu bora zaidi ya hilo. Hilo lingekufanya mwabudu sanamu bila shaka kama ibada ya sanamu ilivyo, mna miungu mitatu. Inawapasa kuwafanya Mungu yule yule, hiyo si miungu mitatu, ni afsi tatu za Mungu yule yule. Ona, Mungu alitumika

katika ubaba, akatumika katika uwana, kisha sasa anatumika katika nyakati za Roho Mtakatifu. Ni Mungu yule yule.

487 Hiyo ndiyo sababu tuliagizwa kubatiza kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; kwa sababu, si kwa jina la . . . Kwa *Jina*, si kwa majina; si kwa majina, au kwa jina la Baba, kwa jina la Mwana, na Roho Mtakatifu; bali “kwa Jina La Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.” Ona, kumtambua Mungu yule yule kuwa Kristo. Ona, hivyo ndivyo Yeye alivyo, hamna njia nyingine yo yote. Ona? Na Maandiko . . .

488 Ndi—ndipo basi ikiwa ufunuo wetu si sahihi, basi Petro pamoja na mitume wengine wote walifundisha jambo lisilo sahihi; kwa kuwa kila mtu katika Biblia alibatizwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Hakuna hata mmoja aliyepata kubatizwa katika “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” ni fundisho la Katoliki. Naweza kuwathibitishieni kwa maneno yao wenyewe, na kamusi yao wenyewe, na kadhalika. Ni imani ya Katoliki na si—na si fundisho la Biblia. Wala hapana mtu . . .

489 Hata Mfalme wa Uingereza alibatizwa kwa Jina Lake Yesu Kristo. Yapata miaka mia sita baada ya kifo cha mtume wa mwisho, wakati ambapo hata haikuwa ikiitwa Uingereza, iliitwa “Nchi ya Malaika.” Hicho ndicho chanzo chake, jina hilo. Yeye alibatizwa kwa Jina Lake Yesu Kristo.

490 Kilichomfanya aongoke, ilikuwa ni zawaridi mdogo. Wakati . . . Kama naweza kukumbuka . . . Si Mtakatifu Angelo. Jina lake lilikuwa nani, ati? Agadabus [Hamna uhakika wa herufi—Mh.], Mtakatifu Agadabus, naamini ndiye. Sina hakika ya jina hilo, sasa. Lakini, haidhuru, yeye alikwenda kule, nao wakapata baadhi ya hawa . . .

491 Waliwaita hao malaika kwa sababu; hao watu pamoja na Waashuru na wengineo walikuwa na sura nyeusi, na hawa Waingereza walikuwa na nywele ndefu, nyeupe, na za ukoka, zenye rangi ya shaba. Wa-Anglo-Saxon, mwajua, macho ya samawati. Nao wakasema, “Walionekana kama Malaika,” na kwa hivyo wakaiita “Nchi ya Malaika.”

492 Naye yu—yule mtumishi wa Bwana akaenda pale na alikuwa akimhubiria mfalme wao, nao walikuwa waketi kwenye meko wazi kubwa. Nilikuwa nikisoma hadithi yake si muda mrefu umepita. Ndipo ndege mdogo akaruka kwenye mwangaza kisha akaondoka, naye mfalme kauliza swali, “Alitoka wapi na ameenda wapi?” Ona? “Yeye aliingia mwangani, nasi tukamwona, kisha akarudi gizani. Je, si hivyo ndivyo mwanadamu aendavyo?” yeye alisema.

493 “Lakini yeye alikuwa nini kabla hajaja hapa?” Kasema yule mhubiri, ona. Hilo likamshika mfalme; na asubuhi iliyofuata, yeye pamoja na nyumba yake wakabatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Naam.

494 Nini basi? Mtu wa kwanza aliyepata kunyunyiziwa ama aliyepata kubatizwa kwa njia nyingine iwayo yote katika jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” alikuwa katika kanisa Katoliki. Kunyunyiziwa kwa kwanza kufanyika, kulikuwa katika kanisa Katoliki. Kumwagiwa maji kwa kwanza kulikofanywa, kulikuwa katika kanisa Katoliki. Kanisa Protestanti kila mara lilibatiza . . . katika Biblia, mitume, kwa kuzika majini katika Jina la Yesu Kristo. Kila mahali. Hebu tafuta mahali pamoja ambapo kulikuwa na kitu kinginecho, ona.

495 Sasa, katika huu, huu wakati mkuu, Wayahudi hawawezi . . . Nilimuuliza huyo rabi, nikasema, “Rabi, ingekuwa vigumu kwako kuamini manabii?”

496 Akasema, “Naamini manabii.”

497 Nikasema, “Katika Isaya 9:6 alimaanisha nini, ‘Kwa ajili yetu mtoto amezaliwa.’ Alikuwa akinena kuhusu nani?”

498 Yeye akasema, “Alikuwa akinena kuhusu Masihi.”

499 Nikasema, “Basi Masihi atazaliwa?”

500 “Naam, atazaliwa.”

501 Nikasema, “Basi kama hana budi kuzaliwa, yeye ana . . . atakuwa na mama.”

502 “Naam, hana budi kuwa na mama. Wala hana budi kuwa na baba, pia,” akasema.

503 Nikasema, “Bila shaka. Basi, ingekuwa vigumu kwako kuamini kwamba hilo halinge . . . kwamba Mungu, Yehova Mkuu aliyefungua Bahari ya Shamu, angemzaa huyu mwana kwa uzazi wa usio na dhambi?” Ona?

504 Yeye akasema, “Ila huwezi kumfanya miungu mitatu.”

505 Nikasema, “Yeye si miungu mitatu.” Nikasema, “Masihi atakuwa na uhusiano gani na Mungu?”

506 Akasema, “Yeye atakuwa Mungu.”

507 Nikasema, “Sasa umelipata. Yeye ni Mungu.” Ndivyo hasa.

508 Ndipo yeye akajaribu kuniambia, akisema, “Vema, mtu huyu alikuwa mwizi, huyu Yesu wa Nazareti. Yeye alikuwa mwizi.”

509 Nikasema, “Rabi, alikuwaje mwizi?”

510 “Vema,” akasema, “Maandiko yenu wenyewe yalisema kwamba ‘Yeye aliingia katika shamba la ngano siku ya Sabato, akachukua ngano.’”

511 Nikasema, “Naam, rabi, wafahamu vema zaidi . . . zaidi juu ya Maandiko kuliko hivyo. Maandiko yenu husema ni halali, ‘Ni halali kwa mtu kwenda na kula ngano kadiri atakavyo, ila asiweke mfukoni mwake aende nayo.’ Sheria zenu wenyewe,

512 Naye akasimama pale kidogo, a—a—aliliamini, kwa kuwa a—alishuhudia. Akasema, baada ya muda mfupi, akasema,

“Vema, nini—nini ilisababisha macho ya John...” Kasema, “Ulifanyaje?”

513 Nikasema, “Kwa Jina la Yesu Kristo.”

514 “Uhu.” Ha—hakujua; kasema, “Vema, huwezi kumkata Mungu katika vipande vitatu.”

515 Nikasema, “Yeye alikuwa Yehova aliyefanyika mwili, rabi. Yeye... Hivyo ndivyo alivyokuwa, alikuwa Yehova katika mwili. Jina Lake la kibinadamu, hilo ndilo lililokuwa Jina la ukombozi, kwa maana hakuna jina jingine liwalo lote walilopewa chini ya Mbingu ambalo mwanadamu aweza kuokolewa kwalo, ila tu kwa hilo Jina la kibinadamu la ukombozi: Bwana Yesu Kristo. Naam. Yeye alikuwa Mungu, Yeye ni Mungu, Yeye atakuwa milele Mungu, ni kweli hasa, Bwana Yesu Kristo.”

516 Sasa, naamini kuwa kanisa la Mataifa hivi punde lita... kule kutimilika kwa ule mwili wa lile kanisa la Kimataifa. Ile milango kati ya... Yesu alisema, katika Mathayo 24, (nitachukua hilo Andiko moja kwa muda kidogo.) Yeye alisema, “Na kuta za Yerusalemu zitakanyangwa hata majira ya Mataifa yatakapotimia.”

517 Sasa tazama. Ilielezwa na Bwana wetu Yesu, katika Mathayo 24, ya kwamba Wayahudi wataangamizwa. Danieli alisema, manabii wa kale, yeye alisema kwamba kutakuwa na majuma sabini ambayo yamekusudiwa kwa Wayahudi. Kisha Masihi angekuja (yule Mtawala) na angetabiri katikati ya lile juma la sabini, ambalo lilikuwa ile miaka saba, yeye angekatiliwa mbali katikati yake. Tazama jinsi ilivyokuwa kamilifu. Yesu alihubiri kwa miaka mitatu na nusu kisha akasulubiwa. Lakini kunayo miaka mitatu na nusu ambayo imekusudiwa kwao, hao Wayahudi. Haina budi kuweko.

518 Sasa kama utachukua Ufunuo, sura ya 7, Yohana aliona wale Wayahudi mia na arobaini na nne elfu wametiwa muhuri, wa yale makabila kumi na mawili ya Israeli. Mnafahamu ninalomaanisha? Ambayo yangali bado yatatendeka hivi punde, itatendeka.

519 Basi tazama jinsi ilivyo nzuri, kabla hatujafunga sasa. Tazama jinsi—jinsi inavyozunguka. Sasa, hao Wayahudi wamepofushwa.

520 Sasa, hawa Wayahudi hapa, wengi wao hapa, wana... mwajua walivyo, ndio wenye utajiri wa ulimwengu. Nao ni—watu wapenda fedha sana, na hilo tu ndilo unaloweza kuona kwao, ona; wenye kiburi sana, na wasiojali, nao hawasikii. Lakini hao sio wale Yeye alikuwa akinena habari zao, kama utachunguza.

521 Basi, Mataifa... Sasa tazama, bado kungali miaka mitatu na nusu kwa ajili ya hawa Wayahudi. Naam, Yesu alisema kuwa mji wa Yerusalemu utakanyagwa na Mataifa hata majira

ya Mataifa... (sasa, ... ninyi watu msioamini katika majira, na hilo, je?)... Hata majira ya Mataifa yatakapotimia. Na majira ya Mataifa yatimiapo (wakati wa Mataifa umekwisha), ndipo mji ule utarudishiwa tena Wayahudi. Kisha Yesu akaendelea kusema kizazi kile... Kasema, "Mnapotoka nje na kuona mtini uishapo kuchipuka, na miti mingine imekwisha kuchipuka," kasema, "mwajua wakati wa mavuno umekaribia." Kasema, "Nanyi kadhalika, myaonapo mambo haya yakitimia, tambueni ya kwamba wakati u karibi, mlangoni; amini, nawaambiani, kizazi hiki hakitapita, hata hayo yote yatimie."

⁵²² Naam, wao walitazamia hayo katika kizazi hicho, "Hayo ndiyo aliyokuwa akinena." Sivyo kabisa!

⁵²³ Sikiza! Yeye alisema, "Kile kizazi kitakachouona mtini ukichupuka." Sasa tazama, Yeye alisema, "Mtini, na miti mingine yote." Naam, yaani, "Kungekuwa na ufufuo wa ulimwengu wote wakati huo." Sasa tazama huu unabii, jinsi unavyotekelezwa na kupatana kabisa. Sasa tazama. "Miti mingine yote ikichipuka, ikifufuka." Mti, unapochipuka, unafufuka. Sivyo? Sasa, kila mtu anajua, mwalimu wa kinabii, ya kwamba mtini daima umekuwa Myahudi. Tunajua hayo. Ni Myahudi. Sasa hao...

⁵²⁴ Na mtazame Yoeli, aliposhika hatamu, alisema, "Yaliyosazwa na tunutu, yameliwa na madumadu, yaliyosazwa na madumadu yameliwa na nzige; na yaliyoliwa na nzige..." Ukichunguza, huyo ni ndudu yule yule, vipindi mbalimbali: tunutu, madumadu, nzige. Ni mdudu yule yule, ni vipindi mbali mbali tu vya maisha yake. Sasa tazama, mdudu yuyo huyo alianza kuula ule mti wa Kiyahudi kule nyuma, akauangusha, na akaanza kula na kula na kula na kula hadi akafikia kwenye shina; Bali hatimaye akasema, "Nitawarudishia," asema Bwana, "miaka yote iliyoliwa na tunutu. Nami nitawafanya watu wayafurahie." Mnaona? Sasa, mti ule umekwisha kuliwa. Mataifa wamepandikizwa mle, naam. Vema, yatupasa tuzae matunda.

⁵²⁵ Basi wakati wa mwisho utakapokuja, tunapokaribia mwisho (kama naiona sahihi), Injili ni: kunapaswa kuwepo na ufuo mkuu.

⁵²⁶ Naam, je, mlijua kuwa bendera ya Wayahudi ndiyo bendera ya kale zaidi ulimwenguni? Na haikutumika kwa miaka elfu mbili, zaidi ya hiyo, yapata miaka elfu mbili na mia tano. Ile bendera ya Wayahudi, ile nyota yenye pembe sita ya Daudi, haikupeperushwa kwa miaka elfu mbili na mia tano; tangu ule uhamisho wa—wa Babeli. Na sasa, kwa sababu ile Milki ya Kirumi iliwatawala (kisha Masihi akaja na wakamkataa), kisha wakatawanyika kwenye pepo nne za dunia. Bali je, mwajua, Mei 6, 1946, bendera ile ilipandishwa tena juu ya Yerusalemu? Je, mwajua, Mei 7, 1946, Malaika wa Bwana alinitokea

(siku iliyofuata) juu hapa, na akanituma ulimwengu kote kuleta ufufuo? Asubuhi iliyofuata! Bendera hiyo ilipopandishwa Yerusalemu kwenye machweo ya jua alasiri hiyo, Malaika wa Bwana alinitokea hapa Marekani wakati uo huo. “Mwonapo mtini na miti mingineyo ikiisha kuchipuka!”

⁵²⁷ Wangapi wanakumbuka ile Nyota iliyoning’inia humu kwenye Mto Uhio, miaka mingi iliyopita, Yeye aliposema... Picha yake ingali hapa bado, Yeye aliposhuka. Kasema, “Ujumbe Wako utatangulia kule kuja kwa pili, kama tu Yohana alivyoondoka akaja kama mtaangulizi wa kule kuja kwa kwanza.” Na, tazama, kote duniani, kumetokea ufufuo. Maelfu mara elfu mara elfu, na ufufuo mkuu.

⁵²⁸ Washika sheria wote, na wengineo mbalimbali kote nchini, pamoja na makanisa makubwa, “Siku za Billy Sunday zimekwisha.” Bali walipoona kanisa likianza kupata ufufuo (watu wa kawaida), iliwabidi kufanya kama haidhuru. Charles Fuller angepachukua mahali hapo, bali alikuwa mzee sana; kwa hivyo wakaenda na Billy Graham. Kisha Mungu akamchukua Billy Graham... au kanisa Baptisti likamchukua, nao watu wakamfuata. Wala Billy Graham hafikii nusu ya Ndugu Neville kwa kuhubiri, tukinena habari za kuwa mhubiri, si kwa... la, sivyo kamwe. Lakini ni nini? Iliwabidi wafanye hivyo, ni muungano, na kila mtu anauunga mkono, kukusanyika hapo. Billy anasema jambo lile lile. Ona, iliwabidi kutenda hivyo. Ilibidi itendeke likatimie Neno la Mungu. Hawakuwa na Roho wakamkusanyikie, kwa hivyo ikawabidi kuchukua Neno na kulikusanyikia; kwa hivyo wakatenda hayo. Billy ni mhubiri wa Neno, na rafiki sana, nao wakakusanyika pale, kwa hivyo hiyo ikaweka watu wote baridi na wa kidesturi katika mkusanyiko wao. Kisha kile Kiembe cha kimbinguni, pamoja na uponyaji wa Kiungu, na nguvu na kutenda kazi na kadhalika, kwa miujiza ya Mungu, viliweka hili... Kanisa, Bibi-arusi atakayenyakuliwa na mwenye mafuta katika taa yake, vikampa ufufuo. Ona? Kisha kanisa baridi la kidesturi likapata ufufuo wake. Na humu mna Israeli na ufufuo wao.

⁵²⁹ Nina sinema mle nyumbani mwangu hivi sasa, *Usiku wa Manane Kasoro Dakika Tatu*. Nasi tuna picha ya hao Wayahudi wakiingia. Wakiingia; mliiona katika gazeti litwalo *Look*. Na meli, zimejaa, zikija toka Iran na kule chini pia; hao Wayahudi hawakujua kamwe kwamba Yesu aliwahi kuwa duniani, walikwenda chini kule katika ule uhamisho wa Babeli. Hilo tu ndilo walilowahi kujua. Wao walilima... mmeyaona katika gazeti litwalo *Look* au *Life* na mengineyo, ambapo walilima wakitumia vifaa vya miti. Nao walipoona hizo eropleni zikija, walidhani, “Ndiyo hii,” kwa kuwa Mungu aliisha kuwaambia “wangeshuka warudi kule, wangerudishwa Yerusalemu kwa mabawa ya tai.” Naam. Ndio hao. Nao Wayahudi wakasema, “Ndiyo hii.” Wakaingia, nasi tuna picha zao pamoja na sauti

zao, na wakahojiwa; wakitoka kote duniani. Wengine wao humu wamebeba wazee wao mgongoni, hali wali vipofu na viwete. Nao wakitoka kwenye meli zilizotoka mahali mabalimbali ulimwenguni, wakiingia.

530 Nao wakaanza kuokota miamba kwa magunia, toka ardhini; na leo wamepata visima vya maji; ambayo ni nchi ya kilimo iliyo bora sana ulimwenguni. Ile Bahari ya Chumvi ina utajiri mwingi sana kuliko ulimwengu wote uliobaki ukiunganishwa pamoja. Wayahudi wanarudi; imefichwa machoni mwa Mataifa, bali wanachanua maua kama waridi.

531 Waliwaambia hao—hao Wayahudi, walisema, “Je, mnarudi kufia katika nchi ya uenyeji wenu?”

532 Kasema, “Tunarudi kumwona Masihi. Yuko wapi?” Inadhaniwa kuwa yuko hapa.”

533 Ndugu, uonapo mtini unapochanua matawi yake, Yeye alisema, “Kizazi hiki hakitapita hata yote yatimie.” Tazama ufufuo miongoni mwa walio wa kidesturi. Tazama ufufuo wa Kanisa. Tazama ufufuo unaokuja kwa Wayahudi, wanakutarajia kule kuja kwa Masihi. Kanisa lililojazwa Roho, yule Bibi-arusi pamoja na . . . wale wanawali wenye mafuta katika taa zao wataingia kwenye ile Karamu ya Arusi.

534 Wayahudi watasema, “Haya basi. Huyu ndiye Mungu wetu tuliyemngoja.” Hapo ndipo walipo wale mia na arobaini na nne elfu. . . ndipo watu wa Russel walipotatizika. Ndio hao Wayahudi watakaompokea wamesimama pale. Wao walisema, “Huyo ndiye Mungu wetu tuliyemngoja.” Watamwona, waseme, “Uliyapataje? Ulipata wapi majeraha hayo mikononi Mwako?”

535 Yeye akasema, “Niliyapata nyumbani mwa rafiki Zangu.” Naam, “Nyumbani mwa rafiki Zangu.”

536 Yeye atafanyaje? Kanisa la Mataifa litanyakuliwa Utukufuni kisha Bibi-arusi ataozwa kwa Kristo.

537 Yusufu alijijulishaje kwa watu wake? Yeye aliondosha kila Mtaifa mbele Zake. Bila shaka alifanya hivyo. Itakuwaje kwa hao masalia ya huo uzao wa mwanamke? Yule joka alitoa katika kinywa chake maji kufanya vita; Yesu alisema, “wangetupwa kwenye giza la nje, na kutakuwa na kilio na maombolezo na kusaga meno,” ule wakati mkuu wa mateso na majaribu utakaolijilia kanisa la Mataifa.

538 Itakuwaje wakati huo? Kufia imani kutakapowadia, na Mungu amekwisha kutenganisha kila kitu na Wayahudi kule, Yesu atarudi kama Yusufu alivyofanya. Walipomsikia Yusufu, alipowaondosha walinzi wake wote na kadhalika, alipomwona maskini kijana Benjamini na wengineo wakisimama pale, huku wakitubu kwa kumuua Yusufu, na ndiye huyu amesimama mbele zao. Yeye akasema, “Mimi ndiye Yusufu. Mimi ni ndugu yenu.”

539 Ndipo wao wakaona hofu sana, “Yeye ndiye Yusufu. Sasa tunamjua.”

540 Yeye atakaposema, “Mimi ndiye Yesu. Mimi ndiye Masihi.”

541 Watasema, “Jamani, sasa tutaona cha mtema kuni.”

542 Yote yalitendeka kwa utukufu wa Mungu. Haitakuwa Yeye ni... Vema, wangemsika akilia hata kwenye jumba la mfalme Farao, Yusufu akiwalilia.

543 Ngojeni hata Yesu akutane na wale Wayahudi aliolazimika kuwapofusha, kutuachia sisi Mataifa nafasi ya kuingia, huo ndio utakuwa wakati wenyewe, nawaambieni. Yeye atawachukua hao Wayahudi, msijali kamwe, hao Wayahudi wataokolewa. Naam, bwana, ndivyo itakavyokuwa. Basi hayo ndiyo maoni yangu, sioni vinginevyo katika Maandiko. Huna budi kuziweka hizo tatu pamoja, tena.

544 Yakupasa kuwaweka mahali panapofaa wa—wale wanawali wanaolala, li—lile kanisa la kawaida tu, linaloungama, ona. Yakupasa kuliona kanisa... Hayo ni, Wayahudi kwanza, ambao ni watu waliopofushwa tu wanaongojea ukingoni. Yakubidi upige hatua nyingine juu, ambayo ni wale wanawali wanaolala, waliokuwa wazembe, waliondoka tu na kuenda kanisani, na kujiunga na kanisa, ni watu wazuri sana. Kisha yakupasa uone Kanisa, la kiroho, kule Kunyakuliwa, yule Bibi-arusi, akisimama pale. Hao watatu, huwezi... hawachanganyishwi, hata kidogo. Hao wote si wamoja. Si kama Mashanidi wa Yehova wasemavyo kuwa “wale mia na arobaini na nne elfu ni bibi-arusi,” hilo ni kosa. Hao ni Wayahudi, ona. Kuna Bibi-arusi, Wayahudi, mwanamwali aliyelala. Nawe unawachukua wote, na kusema, “Vema, wote watatu wako mahali mbalimbali.” Hao wote, ni tabaka tatu za watu. Naam, hawawezi kuwa hivyo.

545 Ndipo Yesu atakaporudi duniani... Wayahudi, ni akina nani? Matowashi wa hekalu. Basi Yesu atakaporudi, Yeye atakuja *pamoja* na Bibi-arusi, Yesu yuaja mara tatu: Yeye alikuja mara ya kwanza *kukomboa* Kanisa Lake, atakuja mara ya pili *kulipokea* Kanisa Lake, kisha yuaja mara ya tatu *pamoja* na Kanisa Lake. Ona? bila shaka. Kwa hivyo yote ni kuja kumoja kukamilifu, yote ni Mungu mmoja mkuu; aliye mkamilifu; yote ni Kristo mmoja mkamilifu na mkuu; Kanisa moja kuu, kamilifu, ukombozi mmoja mkuu, makamilifu... kila kitu; kinakuwa utatu, bali chote ki ndani ya Mmoja. Ona? Si watu watatu, si watu watatu *hivi*; ni Mtu mmoja tu. Kanisa moja, Mwili mmoja, Kristo mmoja, Bwana mmoja “ndani yenu nyota, na katika ninyi nyote,” na kadhalika hivyo. Wote ni mmoja!

546 Bwana awabariki. Nimewakawisha sana.

547 Bwana akipenda, sasa, nikiweza kuja tena kwa usiku mchache, au Jumapili usiku au kitu fulani kama hicho, iwapo mchumgaji hapa hana cho chote moyoni mwake, nitajaribu kujibu maswali haya hapa. Ee, kuna kadha yaliyo mazuri

sana hapa. Wangapi wangependa kuyasikia? Lo, nayapenda sana. Hebu niyasome tena, upesi sana, kabla sijamrudishia mchungaji ibada.

⁵⁴⁸ Hebu sikizeni hili. [Ndugu Branham ayajibu maswali haya manane yafuatayo katika sehemu ya 3, kuanzia aya ya 668 kama swali nambari 67 na kuendelea hata 74—Mh.]:

Ni wapi ambapo yale mawe ya...Je, yale mawe yanaonyesha nini katika Ufunuo 21? Hilo ni nzuri.

Eleza wale wenye uhai wanne wa Ufunuo 5. Hilo pia ni nzuri.

Wale wazee ishirini na wanne ni akina nani? Hilo ni nzuri pia, ona.

Ile kamba nyekundu ya Mwanzo 38 ilimaanisha nini? Mnakumbuka, yeye alienda akamchukua binti-mkwe wake na kuishi naye kama kahaba; kisha akapiga bei na kujitokeza; ndiposa mtoto alipozaliwa, wakamfunga kamba nyekundu mkononi (yeye aliusukuma nje ndiposa akaurudisha ndani), yu—yule aliyefuata akaja nyuma yake. Ee, hilo ni nzuri; bila shaka ni nzuri.

Je, ni zawadi gani watakazopelekeana kuhusu vifo vya wale mashahidi, katika Ufunuo 11? Hapo ni wakati Musa na Eliya watakaporudi kwa ajili ya ule ufufuo kwa hawa mia na arobaini na nne elfu. **Ni zawadi gani?** Tazama hizo ni nini, hilo ni nzuri sana.

Watakatifu watakuwa wapi baada ya ile miaka elfu moja... (hapa lipo nzuri, wee. Tuta...) **kutawala? watakuwa na mwli wa aina gani?**

Tutahukumuje malaika?

Vipi nywele kuwapendeza malaia katika 1 Wakaorintho? Katika kitabu cha 1 Wakorintho. Mazuri, mazuri sana.

⁵⁴⁹ Bwana awabariki. Natumai Bwana atatuajalia kukusanyika pamoja na kujadili mambo haya, yote ni kwa utukufu Wake. Huenda tusikubaliane juu ya mawazo haya; lakini nitasema jambo moja, iwapo ninyi nyote hupata furaha nyingi kuyasikiza kama nifanyavyo nikinena habari zake, tuna wakati wa ajabu. Amina. Amina.

⁵⁵⁰ Vema, Bwana awe mwema sana kwenu sasa. Msisahau ibada. Mahubiri ya radioni ya Ndugu Neville, sasa, hayo ni kupitia kwa WLRP, Jumamosi asubuhi saa tatu; kwaya ya watu wanne ya Neville, nami nina hakika yatawanufaisha, yafungulieni mkayasikize. Basi nikiweza, nikirudi wakati ufao ama nikiona kwamba nitarudi, nitampigia simu mke wangu; Bwana akiniruhusu niende nikamwone mzee mpendwa Ndugu Bosworth. Ni... Ninyi nyote... nami nitarudi Jumapili usiku.

⁵⁵¹ Bwana awe mwema kwenu sasa. Basi Ndugu, mchungaji, njoo hapa kwa dakika moja hivi; ukachukue ibada. Na:

Msisahau maombi ya kijamii,
Yesu ataka kukutana nanyi pale;
Yeye ataondoa mashaka yenu yote,
Ee, msisahau maombi ya kijamii.

⁵⁵² Je, mnaupenda huo? Wangapi huomba manyumbani mwenu? Hebu tuone, wote...wote...Hilo ni zuri, kaeni karibu na Mungu. Iweni wema, watoto wadogo, Mungu awabariki.

Vema, Ndugu Neville.



Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Kwanza
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume One)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org